mamulakani? Nani akupere eya mamulaka-ya?” 24 Insa akijibu, akiwambira: “Nomi
novyo nukudairini kinu kimoja. Neco mukinijibu, nomi novyo nukwambirani mwenyé

* **21:5** “Mwari wa Ziyoni” ndi wenye kaya ya Yerusalemu. † **21:5** Ona Izaya 62:11; Zagariya 9:9. ‡ **21:9** “Hozana” mana ake “asifiwe”. § **21:13** Ona Izaya 56:7. * **21:16** Ona Zaburi 8:2. † **21:21** Usowezi wa Insa mana ake ndi munu mwenyé kuntumaini Mwenyezimungu sana, tafauti isaka kuwa yonse yakuwa kamba mwango, iye amariza.

mamulaka anitendesa evi vinu-vi.
25 Koziwa ka Yahaya kukiwa ka mamulaka a nani?
A binguni‡ au a wanadamu?" Ewo wakikaidiyana watupu, wakamba: "Epa, tikamba:
'A binguni', atambira: 'Sambi mbena amunkubali?'
26 Na tikamba: 'A wanadamu',
tiwopa wanu konta piya wankubali Yahaya ndi nabii wawo."
27 Basi wakinjibu Insa,
wakimwambira: "Atijiwa!" Na iye novyo akiwambira: "Basi, anta omi sukwambirani
mamulaka a nani anitendesa evi vinu-vi!"

### *Kinyume kuhusu wana wawiri*

28 "Umwe muwonaja? Mwananlume mmoja ákiwa na wana wawiri. Akinfika wak-
wanza, akimwambira: 'Mwanangu, uka rero ukakore kazi masamba.'
29 Iye nakujibu,
kaamba: 'Sisaka!' ikisa akitubiya akuka.
30 Akinfika wapiri, amwambira novire, fala
iye nakujibu kaamba: 'Nukuka Baba!' fala okire.
31 Kati ya wawiri ware, atendire
vyakumwajibu wawa yawo ndi wepi?" Ewo wamba: "Mwana wakwanza." Insa
akiwambira javi: "Nukwambirani kweli kuwa warípisi nsoko na mareba walongorera
mbere yenu kwingira muufalume wa Mwenyezimungu.
32 Kamana Yahaya mwenyé
Koza kaja kwenu kwa njira ya shariya, fala amunkubali. Novyo-sivyo, warípisi nsoko
na mareba wankubali. Na ingawa muwona, mwinsho amutubiye mukinkubali."

### *Kinyume kuhusu masamba a uva na warimi wabaya*

33 "Sikirizani kinyume cengine: Ákiwepo munu mmoja mwenyé nyumba karima
masamba a uva, akijengera sereka. Nkati mwake akisimba pondo, akijenga nnara,
masamba are akiwemisira warimi, akisafíri.
34 Paifikire karibu ya mavuno, kawa-
tuma watumisi wake ka warimi ware, wakatware visumo vyake.
35 Warimi ware
wakiwakola watumisi wake ware: mmoja wakimwibiya, mwengine wakimulaya, na
mwengine wakimpanja na mawe.
36 Mwenyé masamba ire akiwatuma tena watumisi
wengine, wengi futi zaida ya wakwanza ware. Newo wakiwatenda novire.
37 Mwinsho
akintuma mwanawe, akiwaza javi: 'Mwanangu-yu wamwinshimu.'
38 Fala warimi,
pawammonire mwanawe ire, wakambirana watupu: 'Noyu-yu ndi asaka kuriti, tukeni
timulaye, tinriti!'
39 Basi, wakinkola, wakimwefya nyuma ya mpaka wa masamba a
uva are, wakimulaya.
40 Paasaka kuja mwanyewe masamba are, warimi ware awa-
tendaja?"
41 Ewo wanjibu: "Visomi wabaya-wo, awamariza nfululu na masamba-wo
awemisira warimi wengine, wakuwa wakumpa visumo wakati wa mavuno."
42 Insa
akiwambira: "Mwaja? Amufyomire Mandiko§ kuwa:

'Riwe rawafezeyire wajengi,
ndi riwere maalumu ra pamembe ya nyumba.
Kinu-ci akunisha ndi Mola,
na citajabisa mmaso mwetu!'

43 Ndimana nukwambirani kuwa muvuriwa ufalume wa Mwenyezimungu, wapewa
wanu wengine wakupa visumo vya ufalume-wo.
44 Na asáka kugwira julu ya eri
riwe-ri, avunjiwa-vunjiwanga, na warisáka kungwirira onse asaika atenda ufu."
45 Wakulungwa wa dini na Mafarizeu, pawasikire eci kinyume-ci, wereriwa kuwa
kankuwamba ewo.
46 Wakisaka kunfunga, fala wawopa wanu konta wakintula kuwa
nabii wawo.

## 22

### *Kinyume kuhusu jambo ra harusi*

‡ **21:25** Mamulaka ka kulawa binguni sawa-sawa na kwamba mamulaka a kulawa ka Mwenyezimungu. § **21:42** Zaburi 118:22-23.

1 Mara nyengine, Insa akiwajibu akiwasowerera kwa kinyume, akamba: 2 “Ufalume
wa binguni ulandana na nfalume mmoja atengeze harusi ya mwanawe. 3 Katumiza
kuweta warifíwe kujambo, fala awasakire kuja, kú! 4 Akiwatuma watumisi wengine
tena, akamba: ‘Warifíwe wambireni javi: “Onani! Jambo rangu nisa kutengeza,
ng'ombe na micamba isinjiwa futi, vinu piya viwa tayari. Njoni kujambo!” ’ 5 Fala
warifíwe ware awayeriwe, woka vyawo: mmoja koka masamba kwake, mwengine
koka kucuruza vinu vyake, 6 na wengine wakiwakola watumisi ware, wakiwatabisha,
wakiwolaya. 7 Kwa javyo, nfalume ire akikimiwa, akiwatuma masurudadu wake
wakiwolaya visomi ware, nakisa wakitaya moto kaya yawo ire. 8 Ikisa, akiwambira
watumisi wake: ‘Epa jambo riwa tayari, fala warifíwe ndi sawari wanu. 9 Basi ukani
mmasimana-manjira. Piya wamusaka kuwansingana onse warifuni waje kuharusi
kuno.’ 10 Nakulawa watumisi ware woka munjira mure, wawajumanisa wawasi-
manane nawo piya, wabaya kamba wema. Mandowa are warifíwe wakijala bunga-
bunga-bunga.
11 Fala nfalume ire, pengire mmandowa mure kuwawona warifíwe ware, kammona
munu mmoja savarire mavazi a paharusi. 12 Iye akimwambira: ‘Rafiki yangu, kwingira
mwaja emu sauna mavazi a paharusi?’ Iye akinyamala ndu. 13 Basi nfalume ire
akiwambira watumisi wake: ‘Nfungeni maulu na makono, munsukure mumwefye
panja pakisi-po! Epo ndi pooka kurira na kutafuna meno.’* 14 Basi, wengi ndi wetiwa,
fala watondoriwa ndi aba!”

### *Mwaha kuhusu kuripa nsoko*

15 Nakulawa pare, Mafarizeu wakitenda mpango wakunkoresa Insa kwa usemi.
16 Kwa javyo, wakiwapereka wanafunzi wawo pamoja na wa kinya Herodi, wakuka
wakindairi: “Mwanlimu! Tukwijiwa kuwa uwe kuwa múkweli na ufunda njira ya
Mwenyezimungu ka ukweli, aumopa munu asaka kuwa onse, konta aunang'aniza
munu caari. 17 Kwa javyo, tambire mawoni ako. Iwapo haki ya kunripa nsoko
Kaisari † au aipo?” 18 Insa kwa kwijiwa ubaya wawo, akiwambira: “Manafiki, mbena
muniyerera? 19 Nolotereni kuno jarajara ya nsoko-yo.” Ewo wakija nawo jarajara moja,
wakimpa. 20 Iye akiwadairi: “Ewu uso-wu na mandiko-ya a nani?” 21 Wakinjibu: “Vya
Kaisari.” Iye akiwambira: “Basi, ca Kaisari mpeni Kaisari, na ca Mwenyezimungu
mpeni Mwenyezimungu!” 22 Pawasikire javire wakishanga dwaraa. Wakimwasa,
wakuka vyawo.

### *Mwaha kuhusu ukweli wa kufufuka*

23 Noire suku ire, wafika karibu ya Insa Masaduseu, wenye kusema kuwa kufufuka
akupo, wakindairi javi: 24 “Mwanlimu! Nabii Musa kaamba kuwa ikiwa nlume kafwa
bila kupongola naye nkawake, nduye ajuzi anjemele nankweli-yo, filihali apongore
naye, alunga rikolo ra nduye.‡ 25 Kamana kati ya ofwe wana saba, wakwanza kan-
lomba, akifwa. Kwa kuwa aapongore naye mwana, nkawake akilombiwa na nduye.
26 Vikuna novyo na nduye wapiri, na watatu, mpaka wo saba. 27 Mwinsho ya piya
ware, na muka ire akifwa. 28 Sambi, suku ya kufufuka wafwi, aja kuwa nlumake ndi
wepi? Kamana piya ware wânlomba!” 29 Insa akiwajibu, akiwambira javi: “Umwe
mupoteya konta amwijiwa Mandiko wala uwezo wa Mwenyezimungu! 30 Kamana
wafwi pawaja kufufuka awalomba wala awalombiwa, wakuwa kamba malaika wari
binguni. 31 Na nkati ya kufufuka ka wafwi, vyamwâmbiriwe na Mwenyezimungu,
akamba: 32 ‘Omi niwa Mwenyezimungu wa Iburahima na Mwenyezimungu wa Izaki na
Mwenyezimungu wa Yankubu.’§ Amufyomire javi? Basi Mwenyezimungu siyo Nlungu

* **22:13** Mwananlume savarire mavazi a paharusi ire kalaviriwa panja konta aamopire nfalume. † **22:17** Kaisari ákiwa Imperadori (nfalume nkulu) wa Roma na piya inti zire. ‡ **22:24** Ona Kumbukumbu 25:5. § **22:32** Ona Kulawa 3:6,15-16.

wa wafwi, ila wári hai!” 33 Wanu ware, pawasikire javire, watajabu kufunda kwake
kure.

*Mwaha kuhusu ámuri ulu*

34 Mafarizeu, pawasikire kuwa Insa kawanyamaza Masaduseu, wakijumana novyo
pamoja. 35 Kati yawo, mmoja ákiwa mwijiwifu wa shariya. Kwa kumyerera, akindairi
Insa javi: 36 “Mwanlimu, ámuri ulu nkati ya shariya ndi yepi?” 37 Insa akinjibu:
“Mpende Mola, Mwenyezimungu wako, kwa moyo wako piya, kwa roho yako piya
na kwa ankili zako piya.* 38 Eyi ndi ámuri ulu na yakwanza. 39 Na yapiri ilandane
neyi: ‘Mpende mwenziwo kamba vyauripenda mwanyewe.’† 40 Ezi ámuri mbiri-zi
zifindikiriwa Taureti piya na vyawâfundire minabii.”

*Mwaha kuhusu Almasihi na Daudi*

41 Pawajumane Mafarizeu pamoja, Insa akiwadairi, akamba: 42 “Umwe mwanku-
wona mwaja kuhusu Almasihi? Iye mwana‡ wa rikolo ranani?” 43 Ewo wakijibu: “Wa
rikolo ra Daudi!” Iye akiwambira: “Sambi, kwa nguvu za Roho Takatifu, Daudi kamwita
‘Mwenye wangu’. Mwaja? Konta Daudi kaamba:

44 ‘Mola kamwambira Mwenye wangu:
Ikala nkono nriro wangu,
mpaka niwature maaduwi wako sini ya kumaulu kwako!’§

45 Basi, ikiwa Daudi kamwita ‘Mwenye wangu’, aawája mwana wa rikolo rake?”* 46 Na
awerepo munu akidirire kumwambira kinu. Tangu noyo suku-yo, aalawirire tena
wakushubutu kundairi kinu.

# 23

*Insa awalaumu Mafarizeu na wanlimu wa shariya*

1 Sambi, Insa akisowera na junudi ya wanu pamoja na wanafunzi wake, 2 akamba:
“Wanlimu wa shariya na Mafarizeu wekala kiti ca nabii Musa.* 3 Kwa javyo, fulatani na
timizani piya vyawari kukwambirani. Fala asani kufulata vitendo vyawo, konta ewo
cawasema sicawatenda. 4 Wafunga mizigo yakuremera wawatika wanu mmaweya,
fala ewo awasaka kusukula anta na cala kimoja. 5 Ewo watenda vitendo vyawo ipate
wawoniwe na wanu. Wakurisa irizi zawo na wakongeza manyanyavu a malupindo
awo.† 6 Kuwajibu kwikala mahala bora mmajambo na viti vya inshima mmasinagoga‡.
7 Kuwajibu wenshimiwe mwawapita mmabazari, na viwajibu wanu wawete wanlimu.
8 Fala umwe musiwase wanu kukwitani ‘wanlimu’ kamana mwanlimu wenu mmoja
basi, umwe piya muwa munu na nduye, 9 wala mulumwengu-mu musimwite ‘Baba’
munu asaka kuwa onse§, kamana Baba wenu ndi mmoja basi, ári mbinguni. 10 Wala
wasukwiteni mafundi, kamana fundi wenu ndi mmoja basi, Almasihi. 11 Nkulungwa
kati yenu awe ntumisi wenu. 12 Basi munu wakuriremeresa mwanyewe aveyesiwa, na
mwenyé kuriveyesa mwanyewe, aremeresiwa.”
13 Insa akiwambira tena: “Umwe wanlimu wa shariya na Mafarizeu, manafiki,
mulaniwe! Mufunga nryango wa ufalume wa binguni mbere ya wanu. Amwingira

---

* **22:37** Ona Kumbukumbu 6:5. † **22:39** Ona Walawi 19:18. ‡ **22:42** Kigeregu ifasuliwa “mwana”. ‘Mwana’ mana ake siyo kupongola mwana basi, na rikolo piya “mwana”. § **22:44** Ona Zaburi 110:1. * **22:45** Mana ake ndi javi: Mayahudi wakinrindira kuja nlongozi nkulu, ujukulu wa Daudi, wakwitiwa Almasihi, aja kuwavusha wanu wake. Insa kankwamba kuwa iye yeka yake basi kapunda kuwa mwana wa rikolo ra Daudi. * **23:2** “Wekala kiti ca nabii Musa” mana ake wafunda na mamulaka ya Musa. † **23:5** Watenda javire ipate wejiwikane kamba wanu wakushika dini pakulu. ‡ **23:6** Viti vya inshima mmasinagoga na swafa yakwanza nsikiti sawa-sawa. § **23:9** Insa awakataze wanu kuweta wawa zawo “baba” ila kakataza kuweta “baba” wakulungwa wa dini.

wala amuwasa wengire wenye kusakula kwingira. 14 * 15 Umwe wanlimu wa shariya
na Mafarizeu manafiki, mulaniwe! Mupita mbahari na kungulu mumpate munu
munsilimise dini yenu. Fala mukimpata, muntenda kuwa mwana wa Jahanamu mara
mbiri zaida koliko umwe. 16 Umwe walongozi sawawona, mulaniwe! Musema kuwa:
'Alapíra mahala takatifu kilapo-co sico kinu, ila alapíra oru íri mahala takatifu ire,
kilapo-co ndi ca ukweli.' 17 Wajinga sawawona! Epo kinu bora ndi cepi? Oru au mahala
patendesa oru kuwa takatifu? 18 Na musema kuwa: 'Alapíra uralu wa kafara, sikinu,
fala alapíra kafara íri julu ya uralu, kilapo-co ndi cakweli.' 19 Wanu sawawona! Kinu
bora ndi cepi? Kafara au uralu utenderiwa kafara ikiwa takatifu? 20 Basi, alapíra uralu,
alapira uralu na ciri pajulu ya uralu. 21 Alapíra mahala takatifu, alapira mahala-po na
Nlungu ári nopo. 22 Na alapíra bingu, alapira kiti ca utukufu wa Mwenyezimungu na
Nlungu ekare kiti cake.
23 Umwe wanlimu wa shariya na Mafarizeu manafiki, mulaniwe! Muwapa wanu
zaka anta na vinu vya manukatu: safarãu, bizari, na loru. Fala mukwasa vinu bora
pakulu vya shariya: haki, huruma, na uwaminifu. Evi ndi vinu vyamujuzi kutimiza,
musase. 24 Walongozi sawawona! Umwe munsuja bwilimwiti fala mummiza ng'ombe†!
25 Umwe wanlimu wa shariya na Mafarizeu manafiki, mulaniwe! Kiyungu na finga
mukosa kunja, fala nkati mwijala ukoko wa vinu vya unyang'anyi na wájibu mbaya.
26 Nfarizeu sauwona! Kiyungu anza kosa nkati ipate na kunja kusitawi novyo.
27 Umwe wanlimu wa shariya na Mafarizeu manafiki, mulaniwe! Umwe mulanda
makaburi a kupakiwa kinambo akusitawiziwa panja‡, iri filihali nkati muwa makon-
golo a wafwi, mwijala takataka na ucafu. 28 Na umwe novyo, kunja muwoniwa na
wanu kamba wenye shariya, iri filihali nkati yenu wijala unafiki na vitendo vyakuvunja
shariya.
29 Umwe wanlimu wa shariya na Mafarizeu manafiki, mulaniwe! Mujengera mak-
aburi a minabii na mupamba kusitawiza makaburi a wanu wa shariya. 30 Mukwamba:
'Tinainshi enzi za wazee wetu, atingari kujumulana nawo kutawanya damu ya
minabii!' 31 Basi, kwa javyo murolota wanyewe kuwa muwa vining'ini vya ware
wawolaye minabii. 32 Basi timizani kipimo ca ubaya ca babu zenu! 33 Manyoka, wana
wa miraba§! Munyemaja hukumu ya moto wa Jahanamu? 34 Kwa javyo, nukuperek-
erani minabii, wejiwifu, na mafundi. Wamojawapo muwolaya na muwagomezera
mmisalaba, wengine muwacapa viboko mmasinagoga mwenu, na muwenenda muki-
walumbata kila kaya. 35 Kwa javyo ije julu yenu hukumu kwa sababu ya damu ya wenye
shariya itawanyike julu ya ardhi, tangu mwanzo kutawanyika ka damu ya Abeli*,
mwenyé shariya, mpaka na damu ya Zagariya, mwana wa Barakiya wamumulaye
nNyumba Takatifu, kati-kati ya mahala takatifu na uralu. 36 Nukwambirani kweli kuwa
wanu wa eci kizazi-ci, ezi hukumu-zi zíwapata."

### *Insa asowera kuhusu kupenda kwake Yerusalemu*

37 Insa kaamba: "Wanu wa Yerusalemu! Ha, wanu wa Yerusalemu! Wari kuwolaya
na kuwapanja na mawe minabii waperekiwe kwawo! Mara nyengapi yanisakire
kuwakusanya wana wawo kamba uku vyaawakúsanya wanawe akiwafinika mumbawa
zake! Fala umwe amusakire. 38 Aya basi, kaya yenu-yo ikuja kutaduka milembe.

---

* **23:14** Mandiko mengine a mida aipo aya 14: [Umwe wanlimu wa shariya na Mafarizeu manafiki, mulaniwe! Munyang'anya manyumba a manankweli, na kuritula kuwa wanu wema mukilebela duwa nrefu-nrefu. Basi kwa sababu ya javyo, mukuja kuhukumiwa pakulu koliko wengine ware.] Ona Luka 20:47. † **23:24** Kigeregu: "ngamiya". ‡ **23:27** Wakati wa Insa, Mayahudi wakipakanga makaburi kinambo mmaluwanja ipate wanu wasisiyanikire kukumbula. Mida-po munu akikumbula kaburi aakiwa tuhara. § **23:33** Mafarizeu na manafiki manyoka konta maaduwi, sawa-sawa kamba wakulungwa wawo wa mida. * **23:35** Abeli mwana wa Adamu na Hawa. Nang'aniza Mwanzo 4:8.

[39] Konta nukwambirani kweli kuwa amuniwona tena, kulawa sambi-pa mpaka suku†
yamusaka kusema: 'Asifiwe mwenyé kuja kwa zina ra Mola!' "

# 24

*Utuba kuhusu Kiyama*

*Kubushuru ka kudanguka ka Nyumba Takatifu*

[1] Insa, paakilawa nNyumba Takatifu akuka vyake, wanafunzi wake wakinfíka karibu
yake, wakimolotera namuna vyaijengiwe nyumba ire. [2] Insa akiwambira, akamba:
"Mwankuwona evi piya-vi? Nukwambirani kweli kuwa epa hapana riwe ríja kubaki
julu ya riwe renziwe, piya abomoriwa."

*Tabu na kulumbatiwa*

[3] Insa paakikala pamwango wa Mizaituni, wanafunzi wake wakimukira cembe,
wakimwambira: "Tambire vinu-vyo vikuja kukuna rini? Na alamani ya kuja kwake,
suku ya Kiyama?" [4] Insa akiwajibu, akamba: "More-moreni asukuteseni munu, [5] konta
wengi wakuja kwa zina rangu, wakamba: 'Omi ndi Almasihi', na wawatesa wanu
wengi. [6] Umwe mukuja kusikira habari na utesi wa vita. Novyo-sivyo musope. Konta
evyo vinu-vyo lazima vikune. Fala siyo kuwa ndi suku ya Kiyama. [7] Taifa ikuja kutenda
vita na taifa nyengine, ufalume mmoja na ufalume mwenziwe. Cikuja kupita kitikansi
pamoja na njala mahala mwingi mwawenye. [8] Evi vinu-vi piya ndi kamba mwanzo wa
malwazo a kupongola*.

[9] Ewo wakuperekani kutabishiwa na wakuulayani, na mukuja kwiniwa na piya
taifa-zi kwa sababu ya zina rangu. [10] Wengi wakuja kukosiwa, wengi wakuja
kuwapereka wenziwawo kuhukumiwa, na kwinana munu na mwenziwe. [11] Wakuja
kulawirira minabii wengi walongo, wakupita wakiwatesa wanu wengi wawenye.
[12] Kwa sababu ya kongezeka ubaya, kupendana ka wanu wengi kukuja kuwa aba.
[13] Fala mwenyé kuvumirira mpaka mwinsho ndi aja kuvushiwa. [14] Na eyi habari ya
ufalume-yi ikwereziwa ulumwengu nzima, uwé ushahidi mbere ya kabila-zi piya. Epo
ndi paija kufika suku ya Kiyama."

*Tabu ulu*

[15] "Kwa javyo, mukiwona haramu yakutenza uwaribifu mahala patakatifu, kamba
vyaâmbire nabii Daniyeli† (mwenyé kufyoma onse, ereriwe), [16] basi sambi wája kuwa
Yudeya wajuzi watuwirire mmyango, [17] ája kuwapo papala ra nyumba yake onse
asisuke kutwala kinu nnyumba mwake, [18] na ája kuwapo mmasamba onse asiludire
kukaya kutwala mavazi ake. [19] Dambi wemite na maametoto wakowesa kwa ezo
suku-zo! [20] Mulebele duwa ipate kutuwa kwenu kusije kuwa wakati wa kinja au
isiwe suku ya sabadu‡, [21] konta wakati-wo ukuja kuwa wa mashaka pakulu futi,
mashaka saanapita tangu mwanzo wa ulumwengu mpaka sambi-pa, wala aaja kupita
tena. [22] Siwere kunukusiwa nozo suku-zo, aakivuka munu. Fala, kwa sababu ya
watondóriwe§, ezo suku-zo zikuja kunukusiwa. [23] Basi, akilawirira munu akukwambi-
rani: 'Almasihi ndiyu-pa', au 'Ndi ire pare', musikubali. [24] Kamana wakuja kulawirira
maAlmasihi walongo na minabii walongo. Ewo wakuja kutenda alama ulu na maajuza,
wafikirire kuwatesa ware watondóriwe, ikikidirika. [25] Onani, omi nankukwambirani
namapema. [26] Basi akilawirira munu akukwambirani: 'Iye kawa pare, paluwanja

† **23:39** Noyo suku-yo ndi suku ya Kiyama, suku yaaja kwisuka Insa kulawa binguni kuludira mulumwengu.
* **24:8** Mwanzo wa malwazo, nfano wake ndi kamba mwanamuka vyaalwaziwa karibu ya kupongola. Basi, na karibu ya suku ya Kiyama ndi novyo. † **24:15** Ona Daniyeli 11:31; 12:11. ‡ **24:20** Suku ya sabadu ndi suku ya kupumuzika Mayahudi. Suku ya sabadu wakikataziwa na Mayahudi kwenenda. § **24:22** "Watondóriwe" ndi wanu wapendiwe na Mwenyezimungu wapate kunfulata ka ukweli iye pamoja na Almasihi ware.

pare!', musuke noko. Au: 'Kawa nnyumba mure', musikubali. 27 Konta kamba
vyamufahamu kumensa vyakulangaza mashariki mpaka magharibi, ndi vyaasaka kuja
kwisuka Binadamu wa Binguni. 28 Mahala pakufwa nyama apakosa kumota membe*."

*Kuja ka Binadamu wa Binguni*

29 Insa kaamba: "Zikipita suku za mashaka-zo, juwa arija kuwala kukwinukala pi,
mwezi auja kuwala, nondwa zisomoka binguni zikigwa, na nguvu za binguni piya
zitikinyika. 30 Basi ikuja kuwoneka julu ya binguni alama ya kwisuka Binadamu wa
Binguni. Kwa javyo, zilalamika kabila piya za duniya, ikisa wammona Binadamu
akisuka mmawingu binguni, na nguvu pamoja na utukufu pakulu.† 31 Na shauti ulu
ya baramanda, iye awapereka malaika wake. Ewo wakiwakusanya waawatóndore iye,
kwa kila membe nne za duniya, kwanza mwanzo mpaka mwinsho."

*Kinyume ca muti*

32 "Rifyomeseni kwa nfano wa muti wakwitiwa mmongo‡. Mmongo, ukiwa na
vitambi viwisi, ukanza kusipuka masamba, mukwijiwa kuwa kinja cifika futi. 33 Ndi
sawa-sawa novyo. Mukiwona eyo mambo-yo akikuna, ijiwani kuwa Binadamu kawa
karibu, kawa panryango! 34 Nukwambirani kweli kuwa eci kizazi-ci acipita saanakuna
eyo mambo-yo piya. 35 Bingu na ardhi piya vilainika, fala usemi wangu aulainika."

*Hapana ejiwa suku yakuludi Insa*

36 "Na kuhusu suku na wakati wa kukuna novyo vinu-vyo, hapana ejiwa. Awe-
jiwa malaika mbinguni wala Mwana, ila Mwenyezimungu Baba tu basi. 37 Kamana
kamba vyavîkunire wakati wa nabii Nnu, ndi vyavija kukuna pakuja Binadamu.
38 Nozo suku-zo, zikuja kuwa kamba vyazikiwa zire suku saanapita mwanalukaya:
wanu wakirya na wakinywa, wakilomba na wakilombiwa, mpaka suku yengire
nabii Nnu nsafina.§ 39 Wanu awejiwe, mpaka paajire mwanalukaya nkulu, aki-
wakumba piya ware. Basi, novyo ndi vyavija kuwa wakati wa kuja Binadamu.
40 Wakati-wo wakuwapo wanu wawiri mmasamba, mmoja atwariwa mwengine ak-
wasiwa. 41 Wanawaka wawiri wakisaya cakurya, mmoja atwariwa mwengine ak-
wasiwa. 42 Ndimana, rinang'anizíreni konta amwijiwa suku yaasaka kuja Mwenye
wenu*. 43 Tulani kuwa mwenyé nyumba, anejiwa wakati wakuja mwivi, nanga kekala
kunang'anizira, ásase nyumba yake kupapaturiwa. 44 Kwa javyo, umwe novyo muwe
tayari, kamana wakati samuwáza kuwa Binadamu kankuja, akuja."

*Ntumisi wakwamínika na saaminika*

45 "Ntumisi mwaminifu na wa ankili, wakuwa mwenye wake kantula pakaya, awape
wanu wake cakurya na wakati wake, ntumisi-yo nani? 46 Heri ntumisi-yo wakuwa
mwenye wake pakuludi, ansingana akitenda javyo! 47 Nukwambirani kweli kuwa
ntumisi-yo mwenye wake antula kumiliki vinu vyake piya. 48 Fala ntumisi-yo, akiwa
mbaya, kimoyomoyo akwamba, 'Mwenye wangu kakawa kuludi'. 49 Ndimana akwanza
kuwebiya wenziwe ware, akirya na akinywa pamoja na warevi. 50 Mwenye wa
ntumisi-yo paaludi, suku saakinrindira wala wakati sejiwa, 51 iye anhukumu vibaya
futi, na fungu rake antula kundi ra manafiki. Epo ndi paciwa kiriro na kutafuna meno!"

# 25

*Kinyume kuhusu wári kumi*

1 Insa akamba: "Ufalume wa binguni ukuja kulandana na wári kumi, wasukure
kandiyeru zawo, kummwinza mwenye-harusi. 2 Nkati ya ewo wári-wo, watanu

* **24:28** Kigeregu: "marembo". † **24:30** Ona Daniyeli 7:13-14. ‡ **24:32** Kigeregu: "nfigu". § **24:38** Mwanalukaya nkulu kapita enzi za nabii Nnu. Ona Mwanzo 7:15 mbere. * **24:42** "Mwenye wenu" epa mana ake Mwenye Insa.

sawawaza, na watanu wakuwaza. 3 Basi sawawaza ware wasukula kandiyeru zawo,
fala awarisukuze mafuta! 4 Fala wakuwáza ware warisukuza numba za mafuta na
kandiyeru zawo. 5 Kwa kuwa mwenye-harusi ire kakawa kuja, wári ware piya wanza
kusinzira mpaka wakilala. 6 Usiku kati-kati kukinyanguriwa: 'Mwenye harusi kankuja!
Lawani mumpokerere!' 7 Noparepare wári ware piya wakilamuka, wakitengeza
kandiyeru zawo. 8 Sawawaza ware wakiwambira wakuwaza ware javi: 'Timereni
mafuta enu-yo, konta kandiyeru zetu-zi zankuzimika.' 9 Wakuwáza ware wakijibu
wakamba: 'Aripo-ya aatitosha futi kutúmira ofwe nnomwe. Fadari ukani kauzanyiwa
konse mukauze mutumire.' 10 Pawalawire kuka kuuza, akifika mwenye-harusi. Wári
waritengeze ware wakingira naye njambo, nryango ukifungiwa. 11 Ikisa, wári wengine
ware pawaludire wakamba: 'Mwenye, Mwenye, tifungurireni!' 12 Fala iye akiwajibu
akamba: 'Nukwambirani kweli kuwa sukwijiwani.' 13 Basi, rinang'anizireni, kamana
amwijiwa suku wala wakati wakuja Mwenye[*]!"

### *Kinyume kuhusu watumisi watatu*

14 "Wakati-wo ukuja kuwa kamba munu vyaasaka kusafiri, kaweta watumisi wake,
kawagabizi mali zake. 15 Akimpa mmoja talanta[†] ntanu, mwengine talanta mbiri,
na mwengine talanta moja, kila mmoja na uwezo wake. Ikisa akuka vyake. 16 Kwa
mpunde noure, apokerere talanta ntanu ire, kacuruzira na kapata faida ya talanta
ntanu. 17 Apokerere talanta mbiri ire kapata faida ya talanta mbiri. 18 Fala apokerere
moja ire kalawa, kasimba pansi, kafisa nzuruku wapewe na mwenye wake ure. 19 Bandi
ya suku nyingi zawenye, mwenye wa watumisi ire akiludi, wakiwalangirana. 20 Akija
karibu apokerere talanta ntanu ire, akolota nyengine talanta ntanu zire, akwamba
javi: 'Onani Mwenye! Talanta ntanu zamunipere-zi, nezi nyengine ntanu zanipatire
faida.' 21 Mwenye wake ire akwamba: 'Kuwa ntumisi mwema na mwaminifu. Bandi
yakuwa mwaminifu wa vinu aba, sambi nukugabizi vingi. Ingira ufurahi na mwenye
wako!' 22 Akija karibu novyo apokerere talanta mbiri ire, akwamba: 'Mwenye, talanta
mbiri zamunipere, ezi nyengine mbiri zanipatire faida.' 23 Mwenye wake ire akwamba:
'Kuwa ntumisi mwema na mwaminifu. Bandi ya kuwa mwaminifu wa vinu aba,
sambi nukugabizi vingi. Ingira ufurahi na mwenye wako!' 24 Akija karibu novyo
apokerere talanta moja ire akwamba: 'Mwenye, nukwijiwa kuwa kwa munu ngumu,
úvuna mahala sauvyarire, ukusanya mahala sautawanye. 25 Nopa, ndimana nifisa
pansi talanta yako, epa kwanawo talanta yako noire.' 26 Nakujibu mwenye wake ire
ansutumu, amwambira javi: 'Ntumisi mbaya na nfuko! Nivuna mahala sanivyarire,
nikusanya mahala sanitawanye! Ukwijiwa javyo? 27 Ndimana, ukijuzi kutula nzuruku
wangu kubanku, nikija nisingane faida yangu. 28 Basi, mpokeni talanta-yo, mumpe
ire ári nazo talanta kumi ire. 29 Kamana kila mwenyé kuwa nawo, azidi kupewa kwa
wingi. Fala saana, anta aba caári nawo noco, anyang'anyiwa.' 30 Na ntumisi safãi-yo,
ntuwisireni panja pakisi-po. Epo ndi pooka kurira na kutafuna meno."

### *Hukumu ya mwinsho*

31 "Paaja kwisuka Binadamu wa Binguni, na utukufu wake na piya malaika wakuwa
pamoja naye, basi akwikala julu ya kiti ca utukufu wake. 32 Mbere yake ziku-
sanyika kabila piya. Ikisa iye akuja kuwatanusa munu na mwenziwe, kamba nsunga
vyaawatanusa makondoo na mbuzi. 33 Makondoo áwatula upande wa nkono nriro
wake, mbuzi upande wa nkono sonto. 34 Ikisa nfalume ire awambira wári nkono
nriro wake, akwamba: 'Njoni kuno, wenye kujanliiwa na Baba wangu. Ritini ufalume
wamutengezeriwe, tangu mwanzo wa ulumwengu. 35 Kamana inikola njala, munipa
cakurya. Inikola nyotwa, muninywesa maji. Nikiwa myeni, munikaribisha. 36 Nikiwa

[*] **25:13** "Mwenye" epa mana ake Mwenye Insa. [†] **25:15** Talanta ndi nfuko na jarajara.

diki, munipa cakuvala. Nikiwa nlwere, munilwarisa. Nifungiwa nkalaboshu, muja
kuniwona.’ 37 Basi, wanu wa shariya wakinjibu wakamba: ‘Mwenye, rini patuku-
wonire ikukukola njala tukukupa cakurya? Au ikukukola nyotwa tukukunywesa maji?
38 Rini patukuwonire uri myeni tukukukaribisha, au uri diki tukukupa cakuvala?
39 Rini paúkiwa nlwere au nkalaboshu, tikija tukukuwona?’ 40 Nakujibu, nfalume ire
akiwambira: ‘Nukwambirani kweli kuwa, kwa kila kinu camuwatendera wanduzangu
watoto futi-wa mmojawapo‡, epo munitendera omi!’
41 Nakisa kawambira novyo wákiwa upande wa nkono sonto ware: ‘Nitanukeni,
wanu wakulaniwa. Ukani kuri hukumu ya moto wa milele, moto watengezeriwe
Ibilisi pamoja na majini wake§. 42 Konta inikola njala, amunipere cakurya. Inikola
nyotwa, amuninywesire maji. 43 Nikiwa myeni amunikaribishe, nikiwa diki amunipere
cakuvala. Nikiwa nlwere na nifungiwa nkalaboshu fala amujire kuniwona.’ 44 Newo
novyo wakijibu wakamba: ‘Mwenye, rini paikukorire njala au nyotwa, au úri myeni,
au úri diki, au úri nlwere au ufungiwe, ofwe tikitowa kukuhudumu?’ 45 Iye akiwajibu
akamba: ‘Nukwambirani kweli kuwa kila kinu samuntendere wanduzangu watoto
futi-wa mmojawapo, amunitendere omi!’ 46 Basi ewa wakuka kuhukumu ya milele,
fala wenye shariya wakuka kumainsha a milele.”

# 26

*Mpango wakumulaya Insa*

1 Insa paamarize usemi ure piya, wanafunzi kawambira javi: 2 “Mukwijiwa kuwa
ubaki muda wa suku mbiri, ífika suku ya Pashukwa, na Binadamu wa Binguni
aperekiwa akagomezeriwe pansalaba.” 3 Wakati-wo wakulungwa wa dini pamoja
na wazee wa Mayahudi wâjumana pamoja kunyumba ulu ya Kayafa, nkulu wa waku-
lungwa wa dini, 4 wakipanga wantese Insa wankore wamulaye. 5 Fala wakamba:
“Tisinkore suku ya sherehe-yi, isije kulawa vurumãi ya wanu.”

*Insa apakiwa mafuta akunuwira Betaniya*

6 Paafikire Insa Betaniya nyumba ya Ansumani camagundula, 7 mwanamuka mmoja
akinfika karibu yake. Insa pekare akirya, mwanamuka ire asukure munringi mafuta
akuniwira gali sana, akimmiminira Insa nkiswa. 8 Wanafunzi wake ware pawawonire
javire, wakikimiwa, wakamba: “Eyi hasarani-yi? 9 Kamana nanga auzanyiwa nzuruku
mwingi wawenye, wapewa masikini!” 10 Insa pejiwe cawari kuwaza, akiwambira:
“Mbena mumwandibu mwanamuka-yu? Kamana katenda cema kwangu omi. 11 Konta
daima-zi wamasikini wawa pamoja namwe, fala daima amuja kuwa pamoja nomi.
12 Eyu mwanamuka-yu kanimiminira mafuta akunuwira-ya mmwiri mwangu kwa
anzima ya kunitengezera namapema maziko angu. 13 Nukwambirani kweli kuwa
ulumwengu nzima-wu, kila mahala paisaka kwereziwa Habari Ngema, visemiwa
novyo vyaatendire mwanamuka-yu, kwa kukumbukiriwa kwake.”

*Yuda alangela kunzungunuka Insa*

14 Ikisa mmoja wawo kati ya kumi na wawiri ware, wakwitiwa Yuda Shikariyoti,
akuka ka wakulungwa wa dini, 15 akiwadairi: “Nukukugabizini Insa, munipa kinani?”
Ewo wakimpa jarajara talatini za parata. 16 Mwanzo wa noure wakati ure, akisakula
nafasi ya kunzungunuka Insa, awagabizi maaduwi wake.

*Jambo ra Pashukwa*

17 Suku yakwanza jambo ra mikate saitayiwe furumento, wanafunzi wamúkira Insa
wakindairi javi: “Ndepi pausaka tikakutengezere cakurya ca Pashukwa urye?” 18 Neye

‡ **25:40** “Wanduzangu watoto” mana ake wanu wakuriyenyekeya. § **25:41** Kigeregu: “Ibilisi pamoja na malaika wake” fala mana ake malaika-wo ndi majini.

akiwajibu: “Ukani mpaka kaya ulu, ka mwananlume mmoja, mukamwambire javi:
‘Mwanlimu katumiza javi: Wakati wangu uwa karibu kufika. Nukuja kwako kutenda
Pashukwa pamoja na wanafunzi wangu.’ ” 19 Wanafunzi ware wakitenda kamba
vyawatumiwe na Insa, wakitengeza jambo ra Pashukwa rire.
20 Paufikire usiku, Insa kekala pamoja na wanafunzi wake kumi na wawiri kusaka
kurya. 21 Pawakirya, iye akamba javi: “Nukwambirani kweli kuwa piya-mwe mmo-
jawapo anizungunuka.” 22 Wanafunzi ware wakiuzunika pakulu futi. Kwa kila mmoja
akanza kundairi: “Mwenye, unamba omi?” 23 Iye akijibu, akamba: “Ataire nkono wake
pamoja nomi nfinga moja, noyo ndi asaka kunizungunuka. 24 Ndi kweli Binadamu
wa Binguni akufwa kamba vyaasema Mandiko kuhusu iye, fala dambi ire mwenyé
kunzungunuka! Fadari anatowa kupongoriwa noyo munu-yo.” 25 Basi Yuda mwenyé
kunzungunuka, akidairi akamba: “Fala sumi, Mwanlimu?” Insa akinjibu: “Kurisema
mwanyewe.”

### *Insa akwanza Jambo ra Kumbukumbu*

26 Pawakirya, Insa akitwala nkate, nakuntukuza Mwenyezimungu, akimeya akiwapa
wanafunzi wake, akisema akamba: “Twalani mutafune, ewu ndi mwiri wangu.”
27 Nakisa akitwala kikombe, akishukuru novire, akiwapa akisema: “Inywani piya-mwe,
28 kamana eyi ndi damu yangu yakwakikisha kupatana*, damu itawanyike kwa ajili
ya wanu wengi ipate waswamiiwe madambi. 29 Nukwambirani kuwa eci kisumo ca
uva-ci siludira kunywa tena mpaka suku yanisaka kunywa nyipya, pamoja nomwe kati
ya ufalume wa Baba wangu.” 30 Pawesire kwimba nyimbo†, wakilawa wakuka mwango
wa Mizaituni.

### *Insa asema kuwa Peduru akuja kunkana*

31 Ikisa Insa kawambira wanafunzi wake kaamba: “Umwe piya mubugudika nami
usiku wa rero-wu, kamana yaândikiwa javi: ‘Ninlumiza nsunga, nkonjo wa makon-
doo wake utawanyika.’‡ 32 Fala bandi ya kufufuka kwangu, nilongorera Galileya.”
33 Peduru akinjibu, akamba: “Anta ikiwa piya wabugudika nawe, fala omi sishubutu
futi kubugudika!” 34 Noparepare Insa akimwambira: “Nukwambira kweli kuwa usiku
wa rero-wu saanawika kokoriko ntanzi, unikana mara natu.” 35 Peduru akimwambira
Insa javi: “Anta paiwa kuwa tikufwa pamoja, sishubutu futi kukukana!” Na wanafunzi
wengine ware, piya wakisema novire.

### *Duwa ya Insa Getisemani*

36 Ikisa Insa akuka nawo mahala pakwitiwa Getisemani, akiwambira wanafunzi javi:
“Ikalani nopa, omi nukuka mpaka pare nikalebele duwa.” 37 Nakunsukula Peduru
na wana wawiri wa Zebedeyu, akanza kukafilika, akiuzunika. 38 Basi noparepare
akiwambira javi: “Uzúnika pakulu futi moyo yangu, niwa karibu kufwa! Ikalani-pa,
murinang'anizire pamoja nomi.” 39 Akuka mbere aba, akisujudi, akilebela: “Baba
wangu, ikikidirika, kikombe ca nyongo yako-ci§ cinitanuke. Novyo-sivyo, isiwe kamba
vyanisaka omi, ila iwe vyausaka uwe.” 40 Akija ka wanafunzi wake, kawasingana
walarire usingizi, akimwambira Peduru: “Kú, amukidirire kurinang'anizira pamoja
nomi nanga ora moja basi? 41 Rinang'anizireni na lebelani duwa musije kushetwaniwa.
Kamana moyo uwa tayari ila mwiri ndi mwepepe.*” 42 Mara nyengine tena, Insa
akuka akilebela duwa, akamba: “Baba wangu, kamba avikidirika kulavya kikombe-ci
saninywere, basi vitimiziwe vyausaka uwe.” 43 Akija tena, kawasingana wakilala,

---

* **26:28** Ona Kulawa 24:8. † **26:30** Kwa nfano, kaswaida za Zaburi 113-118. ‡ **26:31** Ona Zagariya 13:7.
§ **26:39** Kikombe ca nyongo ya Mwenyezimungu ndi alama ya hukumu yake. Ona Zaburi 75:8. * **26:41** Moyo wa
mwanadamu úsaka kutenda vitendo vyema, ila mwanadamu-yo aana uwezo wakukidiri kutenda evyo vitendo-vyo.

konta maso awaremera usingizi. 44 Nakuwasa, akuka tena akilebela duwa mara
yatatu, akiludira usowezi mmoja noure. 45 Nakisa akiludi akija ka wanafunzi wake,
akiwambira javi: “Mwaja, mungari mukilala, mwankupumula? Tunzani! Ufika wakati
wakuzungunukiwa Binadamu wa Binguni, aperekiwa mmakono mwa wamádambi.
46 Lamukani, tuke vyetu. Onani! Kafika futi mwenyé kunizungunuka.”

### *Kufungiwa ka Insa*

47 Iri Insa kankusowera nawo, sambi akija Yuda, mmoja wawo nkati ya wanafunzi
kumi na wawiri ware. Kaja na junudi ya wanu, waperekiwe na walongozi wa
dini na wazee wa Mayahudi. Wasukure katana zawo pamoja na mipweke†. 48 Ire
mwenyé kunzungunuka, akiwapa alama, akiwambira: “Wanisaka kumpa beju onse,
ndi noyo. Nkoreni.” 49 Noure wakati ure, Yuda akinfika karibu Insa, akimwambira
javi: “Mashikamu, mwanlimu!”, ikisa akimpa beju. 50 Fala Insa akimwambira: “Rafiki
yangu, caulangele kutenda conse, tenda.” Wanu ware, nakufika karibu yake, wakolosa
makono a Insa wakinkola. 51 Sambi mmojawapo wákiwa na Insa ware akolosa nkono,
akisolola jambiya, akinduru ntumisi mmoja wa nkulu wa wakulungwa wa dini,
akinsinja sikiro rimoja. 52 Insa akimwambíra javi: “Tula jambiya yako-yo mahala
mwake, konta wenye kulamusa jambiya onse, iwolaya jambiya noyo. 53 Mwaja?
Udaniza kuwa omi sina uwezo wakunlebela Baba wangu, iye kuniperekera malaika
zaida ya makundi a majeshi kumi na mawiri? 54 Avi sambi, nanga atimiziwa mwaja
Mandiko asema kuwa vikijuzi vikune javi?” 55 Wakati noure, Insa akiwambira junudi
ya wanu ware: “Mulawa na jambiya pamoja na mipweke kuja kunitwala! Omi niwa
mwivi? Suku daima-zi níkikalanga nikifunda Nyumba Takatifu, fala amujire kunikola!
56 Ila kwa piya-vi vikuna ipate atimu Mandiko a minabii.” Basi wanafunzi ware piya
wakimwasa, wakintira.

### *Insa na jumula ya Mayahudi*

57 Wanu wankorire Insa ware wakimukisa ka Kayafa, nkulu wa wakulungwa wa
dini, mahala kawâjumane wanlimu wa shariya pamoja na wazee. 58 Sambi Peduru
akinfulata baidi futi, mpaka nluwani mwa nkulu wa wakulungwa wa dini. Akingira
akikala pamoja na mashikarakanzi apate kwijiwa mwinsho wake. 59 Sambi, jumula ya
wakulungwa wa dini pamoja na wanu piya wa Baraza ya Milandu wakisimanana, wak-
isakula ushahidi wa ulongo wakunkosesa Insa wamulaye. 60 Fala awapatire ushahidi,
ingawa wálawirira mashahidi wengi walongo. Mwinsho walawirira mashahidi wawiri,
61 wamba: “Eyu kasema javi: ‘Omi nikidiri kubomola Nyumba Takatifu ya Mwenyez-
imungu, muda wa suku natu basi níjenga tena upya.’ ” 62 Sambi nkulu wa wakulungwa
wa dini akilamuka, akindairi: “Aujibu kinu ushahidi wawari kukulongopera uwe-wu?”
63 Fala Insa kabaki anyamare. Nkulu wa wakulungwa wa dini ire akimwambira
javi: “Omi nukulapisa kwa zina ra Mwenyezimungu ári hai, tambire kamba kuwa
Almasihi, Mwana wa Mwenyezimungu.” 64 Insa akinjibu: “Uwe ndi vyawamba.
Fala nukwambirani kuwa kulawa sambi-pa, mummona Binadamu wa Binguni ekare
nkono nriro wa Mwenyezimungu, Mwenyé Uwezo, na akisuka julu ya mawingu a
binguni‡.” 65 Basi nkulu wa wakulungwa wa dini akipapula mavazi ake, akamba:
“Iye kakufuru! Tisakula ushahidi wa kinani tena? Munsikira sambi-pa akikufuru.
66 Umwe muwonaja?” Ewo wakinjibu: “Ajuzi aulaiwe!” 67 Sambi wakinsunira kumaso,
wakimwefya soku na malatuma pú-pú-pú, 68 wakamba: “Utibushurira ofwe, Almasihi!
Epa akwibiye nani?”

### *Peduru ankana Insa*

† **26:47** Mpweke ndi muti wakurisukuza munu kuka kuulaya. ‡ **26:64** Ona Zaburi 110:1; Daniyeli 7:13; Matwaya 24:30.

69 Sambi, Peduru kêkala panja nluwani. Ntumisi mmoja mwari akinfika karibu yake,
akimwambira javi: "Nowe novyo úkiwa pamoja na Insa nGalileya!" 70 Fala iye akikana
mbere ya wanu ware piya, akamba: "Cauri kusowera-co, sijiwa!" 71 Nakulamuka pare,
akúka mpaka nkitala, ntumisi mwengine muka akimmona, akiwambira wanu ware,
akamba: "Eyu ákiwa pamoja na Insa nNazareti!" 72 Tena iye akinkana kwa kulapira:
"Eyu munu-yu, simwijiwa!" 73 Mpunde sinkulu wanu wákiwa nopare wakimukira
Peduru, wakimwambira: "Kweli-kwelini, na uwe novyo nkonjo wenu mmoja na
ware, konta kusowera kwako umanyirika!" 74 Noparepare, iye akanza kurilani kuno
akilapira: "Simwijiwa-mi eyu munu-yu!" Mpunde noure, kokoriko akiwika. 75 Sambi
Peduru ire akikumbukira usowezi waâsowere Insa ure kuwa: "Kokoriko saanawika,
unikana mara natu." Basi akilawira panja, akanza kurira pakulu futi.

# 27

### *Insa aperekiwa ka Pilatu*

1 Pakucere subuu namapema, wakulungwa wa dini pamoja na wazee wa Mayahudi
piya wakisikizana kumuulaya Insa. 2 Wakinfunga, wakintwala, wakimpereka ka
guvinadoru Pilatu.

### *Kufwa ka Yuda*

3 Sambi Yuda, ânzungunuke Insa ire, paawonire kuwa kesa kuhukumiwa, akirishuku
pakulu, akiludisa nzuruku wa jarajara talatini za parata ure, akiwapa wakulungwa
wa dini na wazee ware, 4 akiwambira: "Nikola dambi, ninzungunuka munu saana
makosa*." Ewo wakijibu, wakamba: "Ofwe vitiyerireni, eyo shauri yako!" 5 Sambi
Yuda noparepare akitwala jarajara za parata zire, akefyera nNyumba Takatifu, akilawa
akuka akirifungangira. 6 Wakulungwa wa dini wakitwala nzuruku ure, wakamba:
"Ewu nzuruku-wu anta siyo halali kuka kuturiwa ankiba konta nzuruku wa damu."
7 Basi wakisikizana, wakiuza uweru wa nfiyangi viyungu, iwe bushtani ya kuwazika
wayeni. 8 Ndimana, noyo bushtani-yo ikwitiwa "Uweru wa damu" mpaka rero-vi. 9 Kwa
javyo, ukitimiziwa usowezi waâsowere nabii Yeremiya†, akamba:
"Watwala nzuruku wa jarajara talatini wa parata,
beyi yawataire wanu wa Iziraeli kuwa ndi beyi yake,
10 wakimpa nfiyangi-viyungu kuuza naye uweru‡,
kamba Mola vyaânamurire."

### *Insa mbere ya guvinadoru Pilatu*

11 Insa akimisiwa mbere ya guvinadoru, iye akindairi javi: "Uwe kuwa nfalume
wa Mayahudi?" Insa akinjíbu: "Uwe ndi vyauri kwamba." 12 Fala vyawansowerere
wakulungwa wa dini pamoja na wazee ware, iye aajibire kinu. 13 Sambi Pilatu
akindairi: "Ausikira vyawamba-vi kuwa wankukusowerera nowe?" 14 Falakini Insa
aanjibire anta kinu kimoja, guvinadoru akibaki wakushanga pakulu pawenye.
15 Sambi, íkiwa tabiya ya guvinadoru, ikifika suku ulu ya Pashukwa, wanu wakinton-
dolanga nfungwa mmojawapo wawansaka onse afunguriwe. 16 Wákiwa nawo nfungwa
mmoja wakwijiwikana pakulu sana ka ubaya, wakwitiwa Baraba. 17 Kwa javyo, wanu
pawajumane pamoja, Pilatu akiwadairi javi: "Umwe wamunsaka afunguriwe ndi
wepi-pa? Baraba au Insa wakwitiwa Almasihi?" 18 Iye kejiwa kuwa wakulungwa wa
Mayahudi wampereka Insa kwa sababu ya kuntendera wiyana. 19 Visitoshe, Pilatu
ekare kiti cake cakulamula, nkawake akimperekera habari zakwamba: "Usiritaye na
eyo munu wa shariya-yo! Nitabika vinu vingi rero kwa kulota kwa sababu yake."

* **27:4** Kigeregu: "kupoteza damu bila makosa". † **27:9** Ona Yeremiya 32:6-15. ‡ **27:10** Ona Yeremiya 18:2.

20 Wakulungwa wa dini pamoja na wazee, wawashongezera wanu ware wanlebele an-
fungure Baraba, Insa aulaiwe. 21 Sambi, guvinadoru ire akiwadairi wanu ware: "Kati ya
ewa wawiri-wa, wamumpendeleya ninfungure ndi wepi?" Ewo wakinjibu "Baraba!"
22 Mwinsho Pilatu akiwambira: "Sambi Insa wakwitiwa Almasihi nintende mwaja?"
Ewo piya wakijibu: "Agomezeriwe pansalaba!" 23 Iye akiwadairi: "Kakosa kinani
noyu?" Falakini ewo wakizidi kunkuwira, wakamba: "Agomezeriwe pansalaba!"
24 Kwa javyo, Pilatu paawonire kuwa acipo cakukidiri tena ila shonge ya wanu ire
ikizidi, basi akitwala maji, akinawa mmakono mbere ya wanu ware piya, akamba
javi: "Omi-pa sina kosa julu ya damu ya eyu munu-yu. Eyo shauri yenu wanyewe."
25 Wanu ware piya wakijibu: "Damu yake iwe julu yetu na wajukulwetu!" 26 Basi
Pilatu akinfungula Baraba, akiwapa. Fala Insa, bandi ya kucapiwa, wakimpereka
agomezeriwe pansalaba.

### *Masurudadu wanshupa Insa*

27 Ikisa masurudadu wa Pilatu ware wakintwala Insa, wakimwingiza nnyumba ya ki-
falume, wakikusanyika piya masurudadu ware, wakinzunguriza. 28 Wakinvula nguwo,
wakinfinika koti reundu. 29 Nakisa wakipakasa lemba ra miwa wakinvaza nkiswa,
na nlanzi wakinsukuza nkono nriro. Wakitenga malundi mbere yake, wakinshupa,
wakamba: "Mashikamu, nfalume wa Mayahudi!" 30 Wakinsunira mata, wakitwala
nlanzi ure, wakimpanjira nkiswa. 31 Pawesire kunshupa, wakinvula koti reundu rire,
wakinvaza nguwo zake zire, ikisa wankintwala, wakuka wakingomezera pansalaba.

### *Insa pansalaba*

32 Pawakuka munjira, wakisimanana naye mwananlume mmoja wakwitiwa An-
sumani nKireni, wakinshurutisa asukure nsalaba wa Insa.§ 33 Pawafikire mahala
pakwitiwa Gologota (mana ake "Mahala pa Gula ra Kiswa"), 34 wakimpa vinyu yaku-
sanganyiwa na nyongo, fala nakuyeza aasakire tena kunywa. 35 Nakungomezera
pansalaba pare, wakitenda kura namuna yakwawanyirana nguwo zake zire.* 36 Ikisa
wakikala kunnang'anizira paakiwa pare. 37 Pansalaba, julu ya kiswa cake, wakitula
kibawo cakwandikiwa makosa ake a kuwa javi: "EYU NDI INSA, NFALUME WA
MAYAHUDI."
38 Wakiwapo visomi wawiri wakigomezeriwa naye pamoja, mmoja nkono nriro na
mwengine nkono sonto. 39 Wanu wakipita onse wakintukana, wakintikinyira kiswa,
40 wakamba: "Ló! Uwe ubondola na kujenga Nyumba Takatifu kwa muda wa suku natu
basi, rivushe mwanyewe! Kweli-kwelini, kamba kuwa Mwana wa Mwenyezimungu,
isuka pansalaba-po!" 41 Wakulungwa wa dini pamoja na wanlimu wa shariya na
wazee, newo novyo wakinshupa Insa, 42 wakamba: "Kawavusha wenziwe, fala aakidiri
kurivusha mwanyewe! Ngati nfalume wa Iziraeli! Aya sambi, esuke pansalaba-po,
timwamini! 43 Antumainingi Mwenyezimungu! Basi Mwenyezimungu akisaka, an-
vushe, konta kasema javi: 'Omi niwa Mwana wa Mwenyezimungu.' " 44 Na visomi
wagomezeriwe nawo pamoja ware, newo novyo wákintukana.

### *Kufwa ka Insa*

45 Mwanzo wa aduhuri mpaka alhanswiri†, muinti mure piya kunja kukinukala
pi! 46 Kiyasi ca ora ya kenda, Insa akikuwa pakulu, akamba: "Elohi, Elohi, lama
sabakitani?" Mana ake, "Nlungu wangu, Nlungu wangu, sababuni kunasa?" 47 Sambi
wengine wákiwa nopare ware, pawasikire javire, wamba: "Iye kankumwita Aliyasi."
48 Kwa mpunde noure, munu mmoja akituwa, akitwala shiponja, akicoveka nvinagiri,

---

§ **27:32** Munu akihukumiwa kifo akijuzi asukure paweya nsalaba mpaka mahala pawimisiwe mwengine. Insa akisakula kusaidiiwa kinu-co konta kâsokera pakulu konta ya kuhukumiwa pakulu. * **27:35** Ona Zaburi 22:18.
† **27:45** Kigeregu: "ora ya sita mpaka ora ya kenda".

akisomeka munlanzi, akimpa kunywa‡. 49 Fala wengine ware wakamba: "Mwase,
tiwone kamba Aliyasi akuja kunvusha." 50 Basi Insa akikuwa pakulu tena, noparepare
akifwa§. 51 Na pazira ya Nyumba Takatifu* ikanyuka perr kati-kati vipande viwiri, ku-
lawa julu mpaka pansi†. Ardhi ikitetema na mawe makulu-makulu akatuka-atukanga
bwa-bwa-bwa. 52 Makaburi akifunuka, miri mingi ya wanu watakatifu wâfwire, ikifu-
furiwa. 53 Airini, bandi ya kufufuka Insa, wâlawire mmakaburi ware, wakingira nKaya
Takatifu‡, wakiwoniwa na wanu wengi wawenye. 54 Basi, masurudadu wamwikarire
Insa ware pamoja na nkulungwa wawo, pawafahamire kutetema ka ardhi kure pamoja
na vikunire vire piya, wopa pakulu futi, wakamba: "Kweli-kwelini eyu ákiwa Mwana wa
Mwenyezimungu!"
55 Nopare mahala pare, wákiwapo wanawaka wengi wawenye, ewo wakiwona wari
baidi. Ewo wânfulata Insa paakilawa Galileya, wakipita wakintumika. 56 Munkonjo
ákiwapo Mariyamu Madalena, Mariyamu mwengine mamaye Yakobu na Yusufu,
pamoja na mama yawo wana wa Zebedeyu.

### *Kuzikiwa ka Insa*

57 Paifikire jironi, akija munu mmoja tajiri nkulu wa kaya ya Arimataya wakwitiwa
Yusufu. Neye novyo ákiwa mwanafunzi wa Insa.§ 58 Nakufika karibu ya Pilatu,
akinlebela apewe maiti a Insa are. Basi Pilatu ire akamuru apewe. 59 Yusufu akitwala
maiti are, akizingiriza kafani, 60 akitula nkaburi rake ripya ratengeze njonga. Ikisa
akipiringisira riwe rikulu panryango wa kaburi rire, akuka vyake. 61 Ákiwepo nopare
Mariyamu Madalena pamoja na Mariyamu mwengine wekala mbere ya kaburi.

### *Kwikarira kaburi*

62 Subuu yake, bandi ya ire suku yakutengeza sherehe*, wakulungwa wa dini na Ma-
farizeu wakijumulana, wakuka ka Pilatu, 63 wakimwambira: "Mwenye, tikumbukira
kuwa nlongo ire ári hai kâsema javi: 'Bandi ya suku natu, nifufuka.' 64 Kwa javyo,
lavya ámuri kaburi rake ririmbisiwe mpaka suku ya tatu, ipate wasije kuja wanafunzi
wake kwiwa maiti ake are, ikisa wawambire wanu kuwa 'Insa kafufuka ka wafwi!'
Ukuja kuwa ulongo wa mwinsho-wu zaida wakwanza†." 65 Pilatu akiwambira javi:
"Walavyeni masurudadu; muwapereke wakekarire kaburi-ro vyamwijiwa vyonse."
66 Basi ewo wakuka wakikarira na wakimatira riwe rire, na wakiwatenga masurudadu
wakinang'anizira.

## 28

### *Kufufuka ka Insa*

1 Bandi ya sabadu, pakucere suku yakwanza ya sumana*, Mariyamu Madalena
na mwanamuka mwengine wakwitiwa Mariyamu wakuka kuwona kukaburi rire.
2 Noparepare, citenda kitikansi pakulu sana, konta laika wa Mwenyezimungu kesuka
kulawa binguni, akija akipingirisa riwe rire, akikarira. 3 Kuwoneka kwake akiwoneka
kamba kumensa, na mavazi ake ákiwa melupa vú kamba bafuta. 4 Na wofi wawo
masurudadu ware wakitetema, wákiwa kamba wafwire. 5 Falakini laika ire akiwambíra
wanawaka ware: "Umwe musope! Konta nukwijiwa kuwa mwankunsakula Insa

---

‡ **27:48** Ona Zaburi 69:21. § **27:50** Kigeregu: "akása roho yake". * **27:51** "Pazira ya Nyumba Takatifu" ikawanya Nyumba Takatifu ipate wanu wengine wasingire Mahala Takatifu Pakulu (mahala pakuwepo Mwenyezimungu Mwanyewe), ila nlongozi nkulu wa dini iye tu basi ákiwa na haki ya kwingira. † **27:51** Vikurire-vyo mana ake ikuwa Mwenyezimungu ndi akunishe. Kwa javyo, njira ya kwingira mahala paMwenyezimungu wafunguririwa wanu piya. ‡ **27:53** "Kaya Takatifu" Yerusalemu. § **27:57** Ona Yahaya 19:38. * **27:62** Suku yakutengeza sherehe íkiwa suku Mayahudi yawakitengeza kusinja micamba ya makondoo kábula ya jambo ra Pashukwa. † **27:64** "(Ulongo) wakwanza" ukwambiwa kuhusu masemo a Insa paambire kuwa iye Almasihi. * **28:1** Wakatí-wo kauli ya Mayahudi, suku yakwanza ya sumana ndi suku ya Jumapiri.

âgomezeriwe pansalaba ire. 6 Epa aapo, kafufuriwa kamba vyaâsemire mwanyewe. Njoni
muwone mahala paâlaziwe. 7 Ikisa ukani upesi, mukawambire wanafunzi wake kuwa
kafufuriwa ka wafwi, nepa kalongorera Galileya. Eko ndi kamuka kummona. Epo nisa
kukwambirani." 8 Basi wanawaka ware wakilawa pakaburi pare upesi-upesi na wofi,
kuno wakifurahi pakulu futi, wakituwa wakuka wakiwambira wanafunzi wake. 9 Kwa
mpunde noure, Insa akisimanana nawo, akiwambira: "Salama!" Newo wakinfika
karibu, wakinkola maulu, wakintukuza. 10 Ikisa Insa akiwambira: "Musope! Ukani
mukawambire wanduzangu woke Galileya, noko waniwona."

*Kwereza ka ulongo ka masurudadu*

11 Wanawaka pawokire vyawo, sambi walawa masurudadu woka mpaka nkaya
mure, wawambira wakulungwa wa dini piya vikunire vire. 12 Basi, wakulungwa
ware wakijumana pamoja na wazee wakitenda mpango, wakiwapa masurudadu ware
nzuruku mwingi wawenye, 13 wakiwambira: "Semani javi: 'Wanafunzi wake waja
usiku wakimwiwa, ofwe tilarire.' 14 Guvinadoru, akisikira mwaha-wu, ofwe tisowera
naye, tukulavyani wasi-wasi." 15 Ewo nakutwala nzuruku ure, wakitenda kamba
vyawafundiwe. Habari ire ikenera piya nkati ya Mayahudi mpaka rero.

*Insa awatuma wanafunzi wake*

16 Sambi, wanafunzi kumi na mmoja ware walawa woka Galileya, pamwango
paâwalaizire Insa. 17 Pawammonire wakintukuza, iri kuwa wengine wákiwa na dana.
18 Insa akiwafika karibu, akiwambira javi: "Piya mamulaka a mbinguni na a duniya
nipewa omi! 19 Basi ukani kabila piya, mukawatende wawe wanafunzi wangu, wozeni
kwa zina ra Baba na Mwana pamoja na Roho Takatifu. 20 Wafundeni wafulate piya vinu
vyanukwamurireni. Kweli, omi niwa pamoja nomwe suku piya, mpaka mwinsho wa
ulumwengu!"

# Habari Ngema yereze
# Maruku

## Mwanzo

Eci kitabu-ci cukolota kuwa Insa ndi Almasihi, Mwana wa Mwenyezimungu. Insa kereza ufalume wa Mwenyezimungu, akiwaponesa walwere, na kafwa kwa kuwombola wenye madambi.

Andíke eci kitabu-ci asowera kuhusu mikonjo mitatu: wanafunzi, junudi ya wanu, pamoja na wakulungwa wa dini. Wakati Insa wafwire pansalaba, surudadu mmoja múRoma ndi áminire kuwa Insa ákiwa Mwana wa Mwenyezimungu.

Ejiwikana andike eci kitabu-ci, fala idaniziriwa kuwa ákiwa mwanafunzi wakwitiwa Yahaya Maruku. Iye kasikira vyaakifundanga Peduru, dalili kwandika ka kitabu-ci kafulata novyo vyaakifundanga-vyo.

### *Yahaya mwenyé Koza atengeza njira ya Insa*

1 Epa ndi payanza Habari Ngema ya Insa Almasihi[*]. 2 Kamba vyavyândikiwe nkitabu
ca nabii Izaya, kuwa javi:

“Ona, mbere yako nimpereka shikarakanzi wangu,
ája kutengeza njira yako.
3 Iye ndi shauti iri kukuwa nlanga, ikamba:
‘Tengezani njira ya Mola, molosereni njira yake.’ ”

4 Shikarakanzi wawenye ndi Yahaya mwenyé Koza. Kaja, kankuwoza wanu kulanga
na kankusema kuwa wanu wajuzi woziwe wolote kuwa watubiya, ipate waswamiiwe
madambi awo. 5 Wanu piya wa makaya a Yudeya na wanu piya wa Yerusalemu
wakuka ka iye, wakoziwa mmuto wa Yordani, wakitubiya madambi awo. 6 Yahaya
ákivalanga nguwo zakupakasiwa na mabururu a ngamiya, na ákirifunganga nkiuno
ukanda wa sambala. Cakurya cake cíkiwa mazorombe na ansali. 7 Iye akihubiri,
akamba: “Kankuja nyuma yangu omi ári nawo uwezo pakulu koliko omi, anta omi sifãi
kwinama kufungula mzizi ya viratu vyake. 8 Omi nukozani[†] kwa maji fala iye akuja
kukozani kwa Roho Takatifu.”

### *Insa akoziwa ikisa ashetwaniwa na Ibilisi*

9 Nozire suku zire, Insa akija kulawa Nazareti ya Galileya, nneye akoziwa na Yahaya
mmuto wa Yordani. 10 Insa, nakulawa mmaji mure, kawona binguni ifunguka, na
Roho Takatifu akimwisukira kamba pomba. 11 Na ikisikirikana shauti kulawa binguni
ikamba: “Uwe ndi mwanangu wanukupenda, niwa radi nawe pakulu.”
12 Mpunde sinkulu, Roho Takatifu kampereka kulanga. 13 Ákiwa kulanga suku
arubaini, akishetwaniwa na Ibilisi. Iye ekáre kati-kati ya manyama wa nnundu, kuno
wakimmudumu malaika.

### *Insa awatondola wanafunzi wake wakwanza*

14 Bandi ya Yahaya[‡] kufungiwa na nfalume Herodi, Insa akúka Galileya, akereza
Habari Ngema ya Mwenyezimungu, 15 akamba: “Wakati ufika! Ufalume wa Mwenyez-
imungu uwa karibu. Tubiyani na pokererani eyi Habari Ngema-yi.” 16 Insa, paakipita
nanyenje ya tanda ra Galileya, kawawona mmaji Ansumani na Andere nduye An-
sumani, wakitaya nyavu kamana wákiwa wavuvi. 17 Insa akiwambira javi: “Njoni

[*] **1:1** Mandiko mengine akongeza: Mwana wa Mwenyezimungu. [†] **1:8** “Kowa” mMandiko ndi kutiwira mmaji, alama yakwanza kuinshi mainsha mapya. [‡] **1:14** Yahaya epa mwenyé Koza.

munifulate, omi nukutendani kuwa wavuvi wakuwavuwa wanu.” 18 Kwa mpunde
noure, nakwasa nyavu zire, wakinfulata.
19 Wenenda kitambo aba, Insa kawawona mungalawa Yakobu mwana wa Zebedeyu
na Yahaya nduye Yakobu wakiwanza nyavu zawo. 20 Mpunde noure akiweta, ewo
wakimwasa Zebedeyu wawa yawo mungalawa nomure pamoja na wakazi wengine,
wakinfulata Insa.

*Insa antuwisa shetwani*

21 Insa pamoja na wanafunzi wake wakuka kaya ulu ya Kafarnaumu, na kila
sabadu Insa ákukanga nsinagoga ya Mayahudi, ákiwafundanga wanu. 22 Ewo wákitajabu
pakulu sana kwa sababu ya kufunda kwake, kamana ákiwafunda vyaafunda munu
mwenyé mamulaka, sairi vyawafunda wanlimu wa shariya. 23 Kwa suku-yo, aki-
kweli-kwelini kuwa ikiwa munu aapongoriwe mara yapiri†, aawona futi ufalume wa
Mwenyezimungu.” 4 Nikodemu akindairi: “Munu ari nkulu, aludira kupongoriwa
mwaja? Vikidirika kuludira mmatumbo mwa mamaye apongoriwe tena?” 5 Insa
akinjibu: “Nukwambira kweli kuwa munu sáapongoriwe kwa maji na kwa Roho wa
Mwenyezimungu, iye engira muufalume wa Mwenyezimungu. 6 Apongóriwe na mwiri
ndi mwiri, na apongóriwe na Roho wa Mwenyezimungu ndi roho. 7 Uwe usishange
vyanukwambire kuwa ibidi mupongoriwe mara yapiri. 8 Mepo ivungira kaisaka konse,
na shauti yake usikira, fala awijiwa ndeyi kailawirira wala kayukirira. Ndi namuna
moja noyo munu wakupongóriwa julu ya Roho wa Mwenyezimungu‡.” 9 Nikodemu
akindairi, akamba: “Vinu kamba-vyo viwaja?” 10 Insa akinjibu akimwambira javi:
“Uwe kuwa mwanlimu nkulu wa waIziraeli. Evi vinu-vi aavikwerera sababuni?

* **2:14** Evi vikuna nluwani mwa wanu Sawari-Mayahudi nNyumba Takatifu. † **2:14** Ikisakikana kukakanya nzuruku nNyumba Takatifu konta wanu wakisakula kutumira nzuruku kuwauza manyama ipate wawatendere kafara. ‡ **2:16** Mana ake: Insa epa akisowera kuhusu mahala pâturiwe kuntukuza Mwenyezimungu wanu Sawari-Mayahudi. Ona Zagariya 14:21. § **2:17** Ona Zaburi 69:9. * **2:21** Mana ake ndi kuwa wamulaya, fala suku ya tatu afufuka. Kwa javyo ndi kulamusa upya nyumba ya mwiri wake. † **2:22** Zaburi 69:9 kambiriwa aya 2:17 julu. ‡ **2:23** Kigeregu: “Wanu wengi wakubali zina rake.” * **3:1** Nikodemu ákiwa nlongozi, nkati ya Baraza ya Milandu. † **3:3** Kigeregu: au “aapongoriwe binguni”. ‡ **3:8** Ona novyo Yahaya 1:13.

11 Nukwambira kweli kuwa vyatijiwa tikwereza, na vyatiwonire tankulavya ushahidi,
fala ushahidi wetu umwe amukubali. 12 Ikiwa nukwambirani vinu vikuna mu-
lumwengu-mu amunikubali, futi nukukwambirani vya binguni mukubalija? 13 Aapo
akweríre kuka binguni sairi Binadamu wa Binguni§ esúke kulawa binguni. 14 Kamba
Musa vyanlamuse nyoka nlanga*, na visakikana novyo kulamusiwa Binadamu, 15 ipate
kila mwenyé kumwamini onse apate mainsha a milele.† 16 Kamana Mwenyez-
imungu kawapenda wanu mulumwengu javi: kawagabizi Mwanawe mmoja noyo
tu basi, ipate kila mwenyé kumwamini asipoteye nfululu fala awe na mainsha a
milele. 17 Konta Mwenyezimungu aampereke Mwanawe mulumwengu-mu kuwala-
mula hukumu wanu, ila kampereka ipate wanu wapate kuvuka julu yake iye.
18 Amwámini aalumuriwa hukumu, ila saamwámini kesa kulamuriwa hukumu futi,
konta aamini caari Mwana mmoja tu basi wa Mwenyezimungu‡. 19 Na javi ndi namuna
vyakujire kulamuriwa hukumu, kwa kuwa ija nuru mulumwengu-mu, fala wanu
wapenda pakulu kisi koliko nuru konta vitendo vyawo vya ubaya. 20 Kamana kila munu
aténda vitendo vya ubaya inkima nuru, na aaja pairi nuru, ipate visiwoneke vitendo
vyake. 21 Fala ire aténda vitendo vyakweli akuja pairi nuru, ipate wanu wawone kuwa
vitendo vyake kankutenda julu ya Mwenyezimungu."

### *Yahaya mwenyé Koza akwamba kuwa Insa ndi bora*

22 Bandi ya evi, Insa pamoja na wanafunzi wake wakija inti ya Yudeya. Akikala nawo
nokure, akozanga wanu. 23 Yahaya novyo akozanga wanu Ainoni karibu ya Salemu,
konta noko ákiwapo maji mengi. Wákijanga wanu, wakoziwa. 24 Epo Yahaya saanamba
kufungiwa nkalaboshu.

25 Sambi, wanafunzi wa Yahaya na Yahudi mmoja wakanza kukaidiyana kuhusu
kutawada. 26 Ewo wakija ka Yahaya, wakimwambira: "Mwanlimu, ire waúkiwa
nawo ng'ambu nyengine ya muto wa Yordani, noire waukílavya ushahidi wake ire,
iye kankoza wanu, na piya wanu wankuka kwake iye!" 27 Yahaya akijibu, akamba:
"Hapana munu apáta kinu sesusiriwe kulawa binguni. 28 Anta nomwe-mwe muwa
mashahidi wangu vyanambire omi: 'Omi siri Almasihi, ila ndi niperekiwe kábula ya
kuja iye.' 29 Ári na mwari-harusi ndi mwenye-harusi, fala rafiki wa mwenye-harusi ndi
arípo epa, na ansikíra akuwa radi pakulu kwa sababu ya shauti ya mwenye-harusi. Kwa
javyo, radi yangu itímu.§ 30 Lazima iye awe bora pakulu, ubora wangu upunguke."

### *Alawíre binguni atipa mainsha meema*

31 Yahaya akizidi kusema, akamba: "Alawíre julu binguni ndi bora koliko piya. Munu
wa mulumwengu-mu wa mulumwengu nomu, na asowera kiulumwengu. Alawíre bin-
guni ndi bora koliko piya. 32 Asikíre na awoníre evyo kankulavya ushahidi, fala hapana
akubali ushahidi wake. 33 Novyo-sivyo, mwenyé kukubali ushahidi wake akwakikisha
kuwa Mwenyezimungu ndi mwenyé ukweli. 34 Konta aperékiwe na Mwenyezimungu
asowera usemi wa Mwenyezimungu, kamana iye akumpa Roho bila kipimo. 35 Baba
ampenda Mwanawe na piya vinu kangabizi mmakono mwake. 36 Ankubali Mwanawe
onse kanawo mainsha a milele. Fala saansikiriza Mwanawe onse aapata mainsha, ila
nyongo ya Mwenyezimungu ikuwa julu yake iye."

## 4

### *Insa asowera na mwanamuka wa Samariya*

§ **3:13** Insa epa akiramba iye mwanyewe. * **3:14** Ona Isabu 21:9. † **3:15** Mana ake: Insa epa akiramba iye mwanyewe paasaka kuja kulamusiwa pansalaba. ‡ **3:18** Kigeregu: "aaminire zina ra Mwana mmoja tu basi wa Mwenyezimungu". § **3:29** Mana ake: Insa ndi mwenye harusi, mwari harusi ndi wenye kumwamini Insa, na rafiki wa mwenye harusi ndi Yahaya mwenyé Koza.

1 Mwenye Insa, pejiwe kuwa Mafarizeu wâsikira kuwa iye kankoza wanu wengi
na ákiwa nawo wanafunzi zaida ya Yahaya, 2 (ingawa Insa mwanyewe siakoza, ila
wakoza ndi wanafunzi wake), 3 iye akilawa Yudeya, akiludira tena Galileya. 4 Ikimbidi
apite Samariya. 5 Basi, akija ire mpaka kaya moja ya Samariya yakwitiwa Sikari,
karibu na uweru Yankubu wampere mwanawe Yusufu. 6 Noparepare úkiwepo nrimbu
waasimbire Yankubu. Ndimana, Insa kwa kuwa kasokera na safari yake, akikala
panrimbu nopare. Nowo wakati-wo íkiwa karibu ya aduhuri.
7 Noparepare, akija mwanamuka mmoja nSamariya kuteka maji. Insa akimwambira:
“Nunu, nimereni maji ninywe.” 8 (Epo iri wanafunzi wake woka kaya ulu kuuza
cakurya.) 9 Mwanamuka nSamariya ire akinjibu: “Umwe muwa Yahudi, omi niwa
nSamariya. Munilebelaja maji a kunywa?” (Akisema javyo kamana Mayahudi na
waSamariya awakipatana.) 10 Insa akinjibu, akimwambira javi: “Kamba ukijiwa
uwezo wa Mwenyezimungu, na ari kukulebela maji a kunywa-yo, uwe ndi ukisaka
kunlebela, na iye nanga kakupa maji a mainsha ako.” 11 Iye akimwambira: “Mwenye,
umwe amuna ndoo, na nrimbu-wu wica pakulu. Sambi maji akunipa mainsha-yo,
musaka kupata ndepi? 12 Ewu nrimbu-wu katipa babu yetu Yankubu. Wákinywanga
iye na wanawe pamoja na mifuwo yake. Sambi, uwe kunzaidi iye?” 13 Insa akinjibu,
akamba: “Eya maji-ya anywa onse iludira kunkola nyotwa tena. 14 Fala munu akinywa
maji animpa omi, ainludira futi kunkola nyotwa kwa milele. Kwasa javyo, maji
animpa omi, kwake iye antadukira kuwa nviriro wakububuka mainsha a milele.”
15 Mwanamuka ire akimwambira: “Mwenye, nimere noyo maji-yo ipate isinikore
nyotwa tena, wala nisije epa tena kuteka maji!” 16 Insa akimwambira: “Uka ukamwite
nlumako, muje onse.” 17 Mwanamuka ire akinjibu, akamba: “Omi sina nlume.”
Insa akimwitikizira: “Kusowera sana kwamba: ‘Omi sina nlume’. 18 Kwa kuwa úkiwa
nawo walume watanu. Na nlume waúri nawo sambi-yo siyo nlumako. Epo kusowera
kweli yako!” 19 Mwanamuka ire akimwambira Insa: “Mwenye, omi niwona kuwa uwe
kuwa nabii! 20 WaSamariya wababu zetu, pawakabudu ndi nowu mwango-wu. Fala
umwe Mayahudi mukwamba kuwa mahala wanu pawajuzi kwabudu ndi Yerusalemu.”
21 Insa akimwambira: “Nunu, namini omi vyanukwambira-vi: ukuja kufika wakati
wakuwa ewu mwango-wu wala Yerusalemu amuja kumwabudu Baba. 22 Umwe
waSamariya mumwabudu nlungu samumwijiwa. Ila ofwe Mayahudi Nlungu wa-
timwábudu timwijiwa, konta kuvushiwa kulawa ka Mayahudi. 23 Fala wakati wanku-
fika, na kweli epa ufika futi, ware wamwábudu ka ukweli wamwabudu Baba kwa
roho, wakifulata ukweli. Kamana Baba nowo ndi wawasakula wamwabúdu iye.
24 Mwenyezimungu ndi roho. Basi wenye kuntukuza iye wajuzi wantukuze kwa roho,
wakifulata ukweli.” 25 Mwanamuka ire akilawa akamba: “Omi nukwijiwa kuwa
Almasihi akuja. Na akija, atambira vinu piya.” 26 Basi Insa akisema: “Omi-pa ndi noyo-
noyoni, omi niri kusowera nawe-mi.”
27 Kwa noure wakati ure, wanafunzi wa Insa wakiludi, washanga kunsingana Insa
akipakanira na mwanamuka ire. Falakini anta mmoja andairire: “Usakulani-pa?”
wala “Mbana kwankusowera naye?” 28 Ikisa, mwanamuka ire akasa nkanfu wake
ure nopare, akiludira ukaya, akuka akiwereza wanu: 29 “Tukeni mukammone munu
anifafanurire piya vyanitendire. Fala noire si Almasihi?” 30 Basi wanu ware wakilawa
nkaya mure, wakuka mpaka kaakiwa Insa kure.
31 Paalawire mwanamuka ire, wanafunzi ware wakinlebela Insa: “Mwanlimu, iryani
ciwa conse-ci.” 32 Fala iye kawambira: “Omi nirya cakurya umwe samwijiwa.” 33 Kwa
javyo, wanafunzi ware wanza kudairiyana watupu: “Fala aapo ajire nawo cakurya
akimpa?” 34 Insa akiwambira: “Cakurya cangu omi ndi kutenda vyaasaka Mwenyez-
imungu anipereke, na kutimiza canitumiwe kutenda. 35 Umwe musoweranga javi:
‘Ibaki tena myezi mine kufika wakati wa mavuno’, sinovyo? Fala omi nukwambirani:

fungulani maso, munang'anize mmamasamba-mo konta mbeyu piya zitokota, zisaka
kuvuniwa.* 36 Mwenyé kuvuna kapata nshahara wake futi, na akusányа visumo apata
mainsha a milele. Kwa namuna-yi, nvyari pamoja na nrimi piya watenderana radi.
37 Konta ewu usowezi-wu wakweli: ‘Mmoja ndi avyála na mwengine ndi avúna.’ 38 Omi
nukuperekani umwe muvune camutowire kukola kazi. Wengine wanza eyi kazi-yi,
umwe mwankufaika ewo cawanzire kutenda.”

39 WaSamariya wengi wakikálanga kaya ulu ire wankubali Insa julu ya ushahidi
wereze mwanamuka ure akamba javi: “Iye kanifafanurira omi piya vyanitendire!”
40 WaSamariya pawajire, wakintafadali kuwa wekare nawo. Basi Insa akikala nawo
suku mbiri. 41 Na wengi wawenye tena wankubali Insa julu ya usemi wake iye
mwanyewe. 42 Ewo mwanamuka ire wakimwambira javi: “Ataminire kwa sababu
vyausowere uwe basi, kamana nofwe wanyewe tinsikira. Epa tijiwa kuwa eyu kweli-
kwelini ndi Nvushi wa mulumwengu-mu.”

43 Bandi ya suku mbiri zekare zire, Insa akilawa akiludira Galileya. 44 (Kusema kweli,
Insa mwanyewe kâlavya ushahidi wakuwa aapo nabii anta mmoja wakwinshimiwa
kwawo.) 45 Paafikire Galileya, waGalileya wampokerera sana-sana, kamana wâwona
piya vyaatendire Yerusalemu pasherehe ya Pashukwa. Kamana ewo novyo woka noko.

### *Alama yapiri yolota vyaári Insa: amponesa mwana wa nkolakazi maalumu*

46 Sambi, Insa akiludira tena Kanaa porovinsiya ya Galileya, kaya yaâtaduse maji
akitenda vinyu. Kaya nyengine, Kafarnaumu, ákiwapo nkolakazi maalumu wa nfalume,
mwanawe ákiwa nlwere. 47 Nkolakazi ire, paasikire kuwa Insa kalawa Yudeya kafika
Galileya, akipita akinsakula. Nakummona akintafadali pakulu pawenye akamba:
“Tuke ukamponese mwanangu, iye kawa karibu kufwa!” 48 Insa akimwambira javi:
“Ikiwa amuwonire alama na maajuza, amushubutu futi kukubali.” 49 Nkolakazi
ire akijibu: “Mwenye, tuke onse sambi-pa, mwanangu saanamba kufwa.” 50 Insa
akimwambira: “Uka, mwanawo-yo apona!” Mwananlume ire akikubali usowezi wa
Insa ure, akiludira kwawo. 51 Munjira paakiteremukira kwawo, akisimanana na
watumisi wake wakimwinza, wakimwambira wakamba: “Mwanenu kapona, kawa
hai!” 52 Iye kawadairi: “Mwanangu kapona wakatini?”

Ewo wakinjibu: “Ijana, ‘uma ora’, homa ndi paimpitire.” 53 Wawa ire kejiwa kuwa
kweli-kwelini mwanawe kapona noure wakati wambiriwe na Insa ure akamba javi:
“Mwanawo kapona!” Kwa javyo, iye pamoja na wajamaa zake piya wakimwamini Insa.
54 Na eyi iwa ndi mara yapiri Insa yaatendire alama ya matajabisa paalawire Yudeya
akija Galileya.

## 5

### *Alama yatatu yolota vyaári Insa: amponesa kitewe*

1 Bandi ya evi, rikiwapo jambo ra Mayahudi, Insa akikwera akuka Yerusalemu.
2 Sambi, Yerusalemu nokurekure, karibu ya nryango wakwitiwa “Nryango wa Makon-
doo”, íkiwapo tanki nkiebraniya wakita “Betizata”, noyo íkiwa na vitololo vitanu. 3 Nkati
ya evyo vitololo-vyo, wákiwapo wanu wengi walwere: wanu sawawona na wakure-
mala na vitewe. 4 * 5 Nopo ákiwapo mwananlume mmoja kálwala myaka talatini na
minane. 6 Insa paammonire aritandikire pansi, na kwa kwijiwa kuwa ákiwapo kure
myaka mingi yawenye, kandairi: “Usaka upone?” 7 Nlwere ire akinjibu: “Mwenye,
maji-ya paaguburiwa, sina anta munu wakunauni kuningiza ntanki-mu. Panikenekeza
kwingira ponse, mwengine arefya omi saninamba.” 8 Insa akimwambira: “Lamuka!

* **4:35** Akiwamba wanu wákiwa tayari kwingira mainsha mapya kunfulata iye. * **5:4** Eyi aya-yi aipo nkati ya mandiko andikiwe sana-sana.

Sukula nanga yako-yo, wenende!” 9 Kwa mpunde noure, mwananlume ire akipona,
akitwala nanga yake ire, akenenda mwanyewe gidi-gidi-gidi.

Suku yaakunire eya maajuza-ya íkiwa sabadu†. 10 Ndimana walongozi wa Mayahudi
wakimwambira mwananlume aponesiwe ire: “Uwe, rero suku ya sabadu! Siyo shariya
kusukula nanga yako-yo.” 11 Fala iye akiwajibu: “Mwananlume aniponese omi ndi
vyaanambire, iye kanambira: ‘Sukula nanga yako-yo, wenende.’ ” 12 Ewo wakindairi:
“Noyo akwambire: ‘Sukula nanga yako wenende-yo’, nani?” 13 Mwananlume apone-
siwe ire aamwijiwe mununi, kamana Insa kalainika, kamana noparepare wákiwapo
wanu wengi wawenye. 14 Airini Insa akisimanana naye tena noire munu ire ku-
luwani ra Nyumba Takatifu, akimwambira: “Wona, uwe kupona! Usikore tena dambi
ipate cisukukune kinu cakofya pakulu!” 15 Ikisa akilawa mwananlume ire, akanza
kuwambira walongozi wa Mayahudi: “Insa ndi aniponese.” 16 Ndimana Mayahudi
wakanza kunlumbata Insa kwa kuwa kâtenda evi vinu-vi suku ya sabadu. 17 Fala Insa
akiwajibu, akamba: “Mpaka rero Baba wangu daima-zi kankukola kazi, nnomi novyo
nankukola kazi‡.”
18 Insa, kwa sababu ya kwamba javire, walongozi wa Mayahudi warimbisa mpango
wakunsakula wamulaye. Aiwere kwa sababu ya kutupa shariya ya suku ya sabadu
noyo tu basi. Ciwakimire pakulu ndi kwa iye kâmba Mwenyezimungu ndi wawaye-
wawayeni. Kwa namuna-yi, akiritula kuwa sawa-sawa na Mwenyezimungu.

### *Mwenyezimungu mamulaka ake akumpa mwanawe Insa*

19 Insa akikola kuwajibu akamba: “Omi nukwambirani kweli kuwa Mwana aatenda
kinu cakuwaza mwanyewe ila atenda caammonire wawaye akitenda. Kamana Baba
caatenda conse, Mwana neye atenda noco. 20 Kweli, Baba ampenda Mwanawe na piya
vinu vyaatenda, amolotera. Visitoshe, vinu vikulu-vikulu vya matajabisa vyakupunda
evi akuja kumolotera ipate piya-mwe mutajabu. 21 Kamba Baba vyawalámusa wafwi
kuwapa mainsha, Mwanawe novyo akumpa mainsha waansaka onse. 22 Kusema kweli,
Baba aanlamula munu, ila kulamula piya kangabizi Mwanawe, 23 ipate wanu piya
wansifu Mwanawe kamba vyawansifu Baba. Ire akatála kunsifu Mwanawe, novyo
kankukatala kunsifu Baba ampereke iye.
24 Omi nukwambirani kweli: asikíriza usemi wangu onse na amwámini anipereke omi,
kanawo mainsha a milele. Iye oka kulamuriwa, ila katupa kifo, kengira futi mmainsha
a milele.
25 Omi nukwambirani kweli kuwa ukuja kufika wakati, na ufika futi, wafwi
wakuja kusikira shauti ya Mwana wa Mwenyezimungu, na wája kusikira-wo wainshi.
26 Kamana, kamba Baba vyaári nawo mainsha iye mwanyewe, iye novyo kampa
mainsha Mwanawe awe nawo iye mwanyewe. 27 Na kampa Mwanawe mamulaka a
kulamula konta iye ndi Binadamu wa Binguni.
28 Musitajabu kukuna kinu kamba-ci, kamana ufika wakati wakuwa piya wari
mmakaburi wasikira shauti yake, 29 na wakuja kulawa. Watendire meema wafufuriwa
wawe na mainsha, na watendire mabaya wafufuriwa wakahukumiwe.”

### *Ushahidi kuhusu Insa*

30 “Omi sitenda kinu mwanyewe. Nilamula kamba vyanisikira. Kulamula kwangu
ndi ka shariya, konta sitenda vyanisaka omi, ila vyaasaka ire anipereke omi.
31 Nikilavya ushahidi kuhusu omi mwanyewe, ushahidi wangu auna faida. 32 Fala
kawapo mwengine alávya ushahidi kuhusu caniri omi. Nukwijiwa kuwa ushahidi
walavya kuhusu omi-wo ndi kweli. 33 Umwe muwapereka wanu ka Yahaya kuku-
dairirani, na iye kalavya ushahidi kuhusu ukweli. 34 Kweli, omi sipokerera ushahidi

---

† **5:9** Sabadu íkiwa suku takatifu ya Mayahudi wanu awakijuzi kukola kazi. ‡ **5:17** Kwa namuna-yo, Insa aritula kuwa iye ákiwa Mwenyezimungu mwanyewe, ákiwa nawo haki ya Mwenyezimungu kutenda kazi daima.

wa wanadamu, ila evi vinu-vi nukwambirani ipate muvushiwe. 35 Yahaya-yo ákiwaka
kamba mwenge vyauwaka ukimwarika. Umwe nlangaza wake mutendera radi muda
aba tu basi. 36 Fala ushahidi wangu nkulu koliko wa Yahaya, kamana vinu Baba vyana-
murire kutenda, novyo-novyoni ndi vyanitenda, vikolota ushahidi kuwa niperekiwa
na Baba. 37 Baba anipereke omi, neye-neyeni alavyanga ushahidi kuhusu omi. Shauti
yake tangu amunamba kunsikira, wala umbo wake amunammona. 38 Usemi wake
auri pamoja nomwe kamana amunkubali wampereke iye. 39 Mandiko Matakatifu
mutunza sana-sana konta mudaniza kuwa nkati yawo mupata mainsha a milele. Noyo
Mandiko-yo alavya ushahidi kuhusu omi! 40 Fala narero, amusaka kuja kwangu
omi kupata mainsha. 41 Sipokerera kutukuziwa ka wanadamu. 42 Fala nukwijiwa
namuna yenu, kuwa nkati yenu amuna pendo ra Mwenyezimungu. 43 Omi nija
mulumwengu-mu kwa zina ra Baba wangu, fala amunipokerere. Ila akija mwengine
wakulavya ushahidi wake mwanyewe, iye mumpokerera. 44 Umwe íri mupokerera
kusifiyana watupu, amuyerera kupata kusifiwa na Nlungu mmoja tu basi, mukubalija?
45 Musidanizire kuwa nukuka kukwerezani ka Baba. Kawapo wakuka kukwerezani
umwe ka Baba, ndi Musa, wamuntumaini umwe. 46 Munankubali Musa, nnomi nanga
munikubali, kamana kandika kuhusu omi. 47 Fala ikiwa vyaandike Musa amukubali,
futi usemi wangu mukubalija?”

# 6

### *Alama yaane yolota vyaári Insa: akuvwisa cakurya ciwatosha wanu*

1 Bandi ya evi, Insa kalawa, kaloka ng'ambu nyengine ya Tanda ra Galileya, zina
rengine ra tanda-ro Tiberiya. 2 Wanu wengi wakinfulata konta wâwona alama zake
za maajuza zakuwaponesa walwere. 3 Insa akikwera pamwango, akikala nopo na
wanafunzi wake. 4 Pashukwa, suku ya sherehe ya Mayahudi, íkiwa karibu. 5 Insa
kwefya maso, kawona kundi ra wanu wengi wakija karibu yake, ndimana akindairi
Filipi: “Cakurya cakuwatosha ewa wanu-wa tisaka kuuza ndepi?” 6 Kandairi javyo kwa
kunyerera tu basi, kamana caakisaka kutenda, akijiwa mwanyewe. 7 Filipi akinjibu:
“Jarajara miyateni za parata aziuza mikate yakuwatosha, anta kila munu apate kipande
kimoja-kimoja.” 8 Mwanafunzi wake mmoja wakwitiwa Andere, nyenyeye Ansumani
Peduru, akamba: 9 “Ona, kawapo-pa nnemba mmoja ári nawo mikate mitanu ya tirigu
na inswi mbiri. Fala viwatosha wanu wengi kamba-wa?” 10 Insa akiwambira wana-
funzi wake ware javi: “Wambireni wanu-wo wekare.” Nopare mahala pare íkiwapo
minyani mingi, basi piya ware wakikala bunga-bunga-bunga. Jumula ya wanu ware
kuwawalanga wanawalume tu basi wákiwa alufu ntanu. 11 Basi Insa akitwala mikate
ire, akinshukuru Mwenyezimungu, ikisa akanza kuwatongera wanu wekare ware.
Inswi zire novyo akiwatongera, wakipata kamba vyawakisaka. 12 Bandi ya kwikuta
piya wanu ware, Insa akiwambira wanafunzi wake ware, akamba: “Vipande vibakire-
vyo, lokoterani pamoja tuke, anta kipande kimoja cisipoteye.” 13 Basi ewo wakilokotera
vipande vya mikate mitanu vyawâtafune wanu vikibaki vire, vikijala vikalala kumi
na viwiri. 14 Wanu ware, pawawonire alama yaatendire Insa ire, wakamba: “Kweli-
kwelini, nabii akirindiriwa kuja mulumwengu-mu ndi noyu!” 15 Insa kejiwa kuwa
wákiwa tayari kuja kunkola makunje, wantawaze kuwa nfalume. Ndimana akilawa
tena yeka yake, akiludira kumwango.

### *Alama yatanu yolota vyaári Insa: akwenenda julu ya maji*

16 Paifikire jironi, wanafunzi wa Insa wakiteremukira kutanda. 17 Wakingira
mungalawa, wakilokera Kafarnaumu. Juwa riswa kunja kwinukala pi, na Insa akiwa
saanamba kuja pawákiwa pare. 18 Ntanda mure mutimbuka kwa kuwa ikivunga mepo
nyingi ti-ti-ti. 19 Wanafunzi ware, pawakivuta magasiya kitambo ca kilometuru ntanu

au sita, noparepare wammona Insa akija akenenda julu ya maji, akifika karibu ya
ngalawa ire! Ewo wakisusuka! [20] Fala Insa akiwambira: "Ndumi! Musope kinu!"
[21] Basi, wakisaka kumpokerera mungalawa mure. Kwa mpunde noure, wawona wári
nlufuko kaya yawakuka ire.

*Insa ndi nkate wa mainsha*

[22] Subuu yake, wanu wabakire ng'ambu nyengine ya tanda ire, wawona kuwa
ibaki ngalawa moja tu basi. Ewo wejiwa kuwa mungalawa mure Insa eengire nawo
pamoja na wanafunzi ware engire nawo, walawa yeka yawo. [23] Mahala pawâtafune
wanu mikate bandi ya Insa kushukuru pare, karibu pake zikija ngalawa nyengine
za Tiberiya. [24] Wanu ware, pawejiwe kuwa Insa na wanafunzi wake awapo pare,
wakingira mmangalawa mwawo, wakuka Kafarnaumu kunsakula Insa.

[25] Pawansingane ng'ambu nyengine ya ntanda ire, wakindairi: "Mwanlimu, epa
kufika rini?" [26] Insa akiwajibu, akamba: "Omi nukwambirani kweli kuwa munisakula
siyo kwa kuwa muwona alama mojawapo, ila kwa kuwa mutafuna mikate mwikuta.
[27] Musikore kazi kwa anzima ya cakurya camwéfya kunundu, ila shugulikirani cakurya
cukupani mainsha a milele, caakupani Binadamu wa Binguni. Kamana ndi noyo-
noyoni apewe na Mwenyezimungu Baba alama yakwakikisha." [28] Ikisa wanu ware
wakindairi: "Tikitenda kazi za Mwenyezimungu, tíjuzi titende kinani?" [29] Insa akiwa-
jibu, akamba: "Kazi za Mwenyezimungu ndi javi: munkubali waampereke iye." [30] Kwa
javyo, wandairi: "Alama yautenda tiwone tukukubali, kinani? Kwankutenda kinani?
[31] Babu zetu wârya nlanga mikate yakwitiwa manã. Kamba vyavyândikiwe mMandiko*:
'Iye mikate ya mbinguni kawapa warye.' " [32] Insa akiwambira tena: "Nukwambirani
kweli kuwa akupereni mikate ya mbinguni siyo Musa. Ila Baba wangu ndi akupani
mikate yakweli ya mbinguni. [33] Kamana cakurya ca Mwenyezimungu ndi ire esuke
binguni, awápa mainsha wanu wa mulumwengu." [34] Wamwambira: "Mwenye, noyo
mikate-yo, tipe daima!" [35] Insa akiwambira: "Omi ndi cakurya ca mainsha. Ája
kwangu omi, ainkola njala tena. Munu anikúbali, ainkola nyotwa tena. [36] Fala
omi nukwambirani kuwa muniwona, novyo-sivyo amukubali. [37] Piya wanigabizire
Baba wakuja kunifulata, na ája kwangu onse, simwefya panja. [38] Kamana nisuka
kulawa binguni sijire kutenda vyanisaka omi mwanyewe ila vyaasaka anipereke omi.
[39] Vyaasaka ire anipereke omi ndi javi: kuwa piya waanipere iye, wasipoteye anta
mmoja, suku ya mwinsho niwafufure. [40] Kamana vyaasaka Baba wangu ndi kuwa
ammóna Mwana, akinkubali iye, akuwa na mainsha a milele. Suku ya mwinsho nomi
ninfufula awe hai kwa milele."

[41] Ndimana Mayahudi wamojawapo† wakanza kunduguda konta kâsema javi: "Omi
ndi nkate wisuke binguni." [42] Ewo wakamba: "Eyu sinoyu Insa, mwana wa Yusufu,
wawaye na mamaye nikamba timwijiwa? Sambi akwamba, 'Nisuka kulawa binguni',
namunani?" [43] Insa akiwajibu: "Asani kuduguda watupu! [44] Aapo munu ája kwangu
omi bila kuvutiwa na Baba anipereke omi. Noyo munu-yo ninfufula suku ya mwinsho.
[45] Nabii mmoja‡ kândika javi: 'Piya wakuja kufundiwa na Mwenyezimungu.' Ndi
kweli kuwa piya wenye kunsikiriza Baba na warifunda kwake, wakuja kwangu omi.
[46] Kusema kweli, aapo munu ammonire Baba sairi ire alawire ka Mwenyezimungu,
ndi ammonire Baba. [47] Omi nukwambirani kweli kuwa mwenyé kwamini kanawo
mainsha a milele. [48] Omi ndi nkate wa mainsha. [49] Wababu zenu wârya manã nlanga,
wafwa nfululu. [50] Eyi ndi mikate isuke mbinguni ipate munu asaka kuwa onse akirya,
asifwe. [51] Nomi-nomini ndi mikate ya mainsha isuke mbinguni. Munu mmojawapo

* **6:31** Ona Zaburi 78:24, 105:40. † **6:41** "Mayahudi wamojawapo" mana ake epa ndi ware wabishána na Insa.
‡ **6:45** Ona Izaya 54:13.

akirya noyi mikate-yi, ainshi milele. Mikate yanukupani wanu wa mulumwengu kuwa mupate mainsha ndi mwiri wangu-wu."
52 Ndimana Mayahudi wakanza kukaidiyana watupu, wakamba: "Eyu munu-yu
vyaatipa mwiri wake tikirya, namunani?" 53 Kwa javyo, Insa akiwambira: "Omi
nukwambirani kweli: ikiwa amurire mwiri wa Binadamu wa Binguni wala amunywere damu yake§, amuwa na mainsha nkati yenu. 54 Mwenyé kurya mwiri wangu
na kunywa damu yangu kanawo mainsha a milele, omi ninfufula suku ya mwinsho.
55 Kamana mwiri wangu ndi mikate yakweli, damu yangu ndi kinywaji cakweli.
56 Mwenyé kurya mwiri wangu na kunywa damu yangu, iye alungana nami, nnomi
nilungana naye. 57 Kamba Baba vyaári hai anipereke omi, nomi niwa hai kwa ajili ya
Baba, ndi novyo anírya omi, akuwa na uhai julu yangu omi. 58 Sambi, eyi ndi mikate
isuke mbinguni. Siyo kamba mikate yawarire wababu zenu ikisa wakifwa. Ila ire árya eyi mikate-yi onse akuwa na mainsha a milele."
59 Vinu-vi ndi vyaasowere paakiwafunda wanu nsinagoga* ya Kafarnaumu.

### *Wanafunzi wajibu usemi wa Insa*

60 Wanafunzi wake wengi, pawasikire usemi ure, wakamba: "Kusikira ewu usemi-wu
urigariga. Epa, asikíre vyaambire-vi, nani?" 61 Insa kejiwa mwanyewe kuwa
wanafunzi wake wankuduguda kuhusu vyaasowere vire, ndimana akiwambira javi:
"Usemi wangu-wu ukutipusani? 62 Ndimana, futi ikiwa mummona Binadamu akikwera kuludira kaákiwa mida? 63 Ampa munu mainsha ndi Roho, mwiri aufãi kinu.
Usemi wanukwambireni umwe ndi roho na ndi mainsha. 64 Fala kati yenu wawapo
wamojawapo sawakubali." (Insa kasowera javyo kamana kawejiwa tangu mida
sawakubali, na kamwijiwa nani ája kunzungunuka kumpereka ka maaduwi.) 65 Iye
akizidi kuwambira akamba: "Ndimana, nukwambirani kuwa aapo munu ája kwangu
omi iye saamuriwe na Baba." 66 Kwa sababu ya kusowera javyo, wanafunzi wake
wengi wakiludira nyuma, awanfulate iye tena. 67 Ndimana Insa akiwadairi mawalii
kumi na wawiri ware: "Nomwe novyo, musaka muke vyenu?" 68 Ansumani Peduru
akinjibu: "Mwenye, tikuka ka nani? Uwe ndi úri nawo masemo wakuwapa wanu
mainsha a milele. 69 Ofwe sambi tukwamini, tikwijiwa kuwa uwe ndi Ntakatifu wa
Mwenyezimungu." 70 Insa akiwajibu: "Umwe kumi na wawiri-mwe, nikamba omi ndi
nukutondoreni? Fala kati yenu alawirira mmoja akuwa shetwani!" 71 Iye akimwamba
Yuda, mwana wa Ansumani Shikariyoti. Kamana Yuda, ingawa ákiwa munkonjo wa ware kumi na wawiri ware, fala kanzungunuka.

# 7

### *Insa paSherehe ya Vitala*

1 Bandi ya vire, Insa akenenda Galileya. Aasakire tena kwenenda makaya a Yudeya
konta wakulungwa wa Mayahudi wakinsakula wamulaye. 2 Ífika karibu suku ya
jambo ra Mayahudi rakwitiwa Sherehe ya Vitala. 3 Ndimana wanduze Insa ware
wamwambira: "Lawa-pa, uka Yudeya, ipate wanafunzi wako newo novyo wakawone
maajuza a utendanga-yo. 4 Kamana munu akisaka kwijiwikana, aajuzi kufisa vitendo
vyake vyaatenda. Ukitenda vinu-vi, rolote baina." 5 Wasema javi konta wanduze
Insa awakinkubali. 6 Insa akiwambira: "Wakati wangu aunafika, ila wakati wenu
umwe-po daima uwa tayari. 7 Wanu wa mulumwengu-mu umwe awakwinani, ila omi
wanina, kwa sababu nilavya ushahidi kuwa vitendo vyawo vya ubaya. 8 Umwe kwerani
muke kusherehe. Omi suka kusherehe-ko konta wakati wangu aunafika nfululu."
9 Nakuwambira javire, iye akibaki Galileya nokure.

§ **6:53** Mana ake: ikiwa amumpokerere Insa na kazi yake. * **6:59** "Sinagoga" mana ake ndi nyumba ya duwa ya Mayahudi.

10 Bandi ya wanduze ware kukwera kuka kusherehe kure, neye novyo akikwera
akuka. Ila okire baina, kóka kwa kurifisafisa. 11 Ndimana Mayahudi wakinsakula
pasherehe pare, wakamba: "Ari, iye noyo kawa ndepi?" 12 Noparepare wanu wengi
wateta kuhusu Insa. Wengine wakamba: "Iye munu mwema" fala wengine wakamba:
"Siyo munu mwema, kankuwatesa wanu." 13 Fala awerepo munu wakusowera baina
kuhusu iye konta wakiwopa wakulungwa wa Mayahudi.

### *Kufunda ka Insa kulawa ka Mwenyezimungu*

14 Kati-kati ya suku za sherehe ire, Insa akikwera kuNyumba Takatifu, akanza kuwa-
funda wanu. 15 Kwa javyo, Mayahudi wakitajabu wakamba: "Eyu mwananlume-yu
kwijiwa evi vinu-vi piya saafundiwe namunani?" 16 Insa akiwajibu, akamba: "Kufunda
kanifunda siko kwangu omi, ila ndi kufunda ka ire anipereke omi. 17 Munu mmojawapo
akisaka atende vyaasaka Mwenyezimungu, basi akwijiwa kuwa eku kufunda-ku ka
Mwenyezimungu au nankusowera kwa mamulaka angu mwanyewe. 18 Asowéra kwa
mamulaka ake mwanyewe asakula kurisifu mwanyewe. Fala ire asakúla kuwa wanu
wansifu ampereke iye onse, akupo kukosa kweli kwake, iye ndi mwenyé ukweli.
19 Musa kakupani Taureti yakufulata, sinovyo? Fala piya-mwe aapo aténda vyaisaka
Taureti. Musakula kunulaya sababuni?" 20 Junudi ya wanu ire ikijibu: "Uwe kuwa na
shetwani! Asakula kukuulaya nani?" 21 Insa akiwajibu, akamba: "Omi nitenda maa-
juza mamoja na piya-mwe mushanga vyanitendire. 22 Novyo-sivyo, Musa kakupani
tabiya ya itani. (Kusema kweli, eyi tabiya-yi sianzire, wanza wababu zenu.) Umwe
mwana nlume muntaya itani anta iwe suku ya sabadu.* 23 Onani, dalili ndi suku ya
sabadu mwananlume yaataiwa itani isifujike shuruti ya Musa. Ndimana, munikimwira
kwa kumponesa munu mwiri nfululu suku ya sabadu sababuni? 24 Musilamure kwa
kunang'anizana kumaso, ila lamulani kwa shariya."

### *Wanu wakaidiyana kuwa Insa Almasihi*

25 Kwa javyo, wanu wamojawapo wa Yerusalemu wakamba: "Mwananlume wawári
kunsakula kumulaya-yu, sinoyu-yu? 26 Mmoneni, iye kankusowera baina wala
awamwambira kinu! Itakuwa wakulungwa wamwijiwa ka ukweli kuwa iye Almasihi?
27 Fala ofwe eyu tikwijiwa kwawo. Paasaka kuja Almasihi, aapo ája kumwijiwa kwawo!"
28 Kwa javyo Insa, paakiwafunda wanu nNyumba Takatifu, kasowera na shauti ulu,
akamba: "Umwe munijiwa? Anta kwetu mukwijiwa? Fala omi sijire epa kwa kusaka
omi mwanyewe. Ila anipereke omi ndi mwenyé ukweli, iye umwe amumwijiwa. 29 Fala
omi nimwijiwa konta nilawa upande wake, iye ndi anipereke." 30 Basi ewo wayerera
kunfunga, fala aapo ankorire nkono, konta wakati wake úkiwa saunafika. 31 Novyo-
sivyo, wanu wengi ware wankubali, wakamba: "Akija Almasihi, atakutenda alama
ulu-ulu zakupunda zaatenda eyu mwananlume-yu?"

### *Insa akwamba kuwa akuka vyake*

32 Mafarizeu wawasikira wanu wakiteta nowu mwaha-wu kuhusu Insa. Ndi-
mana, ewo pamoja na wakulungwa wa dini wawapereka minduna wakanfunge.
33 Noparepare Insa akamba: "Nanawo suku aba futi namwe, ikisa nukuka ka ire
anipereke. 34 Mukuja kunisakula fala amuja kunipata. Mahala kanisaka kuwa omi,
umwe amukidiri kuja." 35 Wakulungwa wa Mayahudi wakanza kudairiyana watupu:
"Noyu mwananlume-yu, ndepi kaasaka kuka ofwe tikisokerera kummona? Apunda
makaya etu akuka inti za Sawari-Mayahudi, akawafunde wanu Sawari-Mayahudi?
36 Paasowera, 'Mukuja kunisakula fala amuja kunipata', mana ake kinani? Na 'Mahala
kaniri omi, umwe amukidiri kuja', manani?"

* **7:22** Shariya isema kuwa kisimana ajuzi engiziwe itani suku ya nane bandi yakupongoriwa.

*Insa awapa wanu maji a mainsha*

37 Suku ya mwinsho ya sherehe, suku iwere ulu, Insa kémira, akisowera na
shauti ulu-ulu, akamba: "Ikiwa kawapo wakunkóla nyotwa, aje kwangu omi, anywe.
38 Mwenyé kunikubali omi, kamba vyaasema Mandiko Matakatifu, 'Nroho yake
ibubuka miviriro ya maji a mainsha.' " 39 Iye akamba javi kuhusu Roho wa Mwenyez-
imungu, kwa ware wenye kunkubali iye waja kumpokerera. Kamana nowo wakati-wo,
Roho Takatifu ákiwa saanamba kuwesukira, konta Insa ákiwa saanamba kutukuziwa.

*Wanu wawanyika kwa sababu ya usemi wa Insa*

40 Wanu wengine pajunudi ya wanu pare, pawasikire ewu usemi-wu, wakamba:
"Kweli-kwelini, eyu mwananlume-yu ndi nabii watikinrindira!" 41 Wengine wakamba:
"Eyu ndi Almasihi." Fala wengine wadairi: "Almasihi atakulawirira Galileya?
42 Mandiko Matakatifu† akwamba kuwa Almasihi ujukulu wa Daudi, sinovyo? Ak-
wamba kuwa akuja kupongoriwa inti Betlehemu kwawo Daudi, sikweli?" 43 Kwa javyo,
kukilawirira kwawanyikana wanu ware kwa sababu ya Insa. 44 Noparepare wengine
wakisakula wanfunge, fala aawerepo wakolosa nkono wake kunkola.

45 Ikisa minduna waludira ka wakulungwa wa dini pamoja na Mafarizeu. Waku-
lungwa wawadairi minduna ware: "Umwe amujire nawo mwananlume ire sababuni?"
46 Ware minduna ware wakamba: "Vyaasowere iye tangu anamba kusowera munu
javire!" 47 Basi, Mafarizeu ware wakiwajibu: "Mwaja? Nomwe novyo mutesiwa?
48 Anta mmoja nkati ya wakulungwa ankubalire? Nfarizeu mmoja ankubalire? 49 Ewu
umati-wu awijiwa shariya za Musa! Ewo walaniwa!" 50 Nfarizeu mmoja nopare
wakwitiwa Nikodemu, âsimanane na Insa kwa suku zipitire, iye akiwambira javi:
51 "Shariya yetu isema kuwa atijuzi kunlamula munu satinamba kunsikira ushahidi
wake, tikijiwa caakosire." 52 Ewo wakijibu: "Epa sambi, nowe novyo kuwa nGalileya?
Unafyoma nanga kuwonerera kuwa nabii mmojawapo wakulawa Galileya aukijuzi
kunrindira." 53 ‡[Basi wakitawanyikana, kila mmoja akuka kwake.

# 8

1 Fala Insa akuka kuMwango wa Mizaituni.

*Mwanamuka mmoja afungiwa kwa sababu ya uzinzi*

2 Alufajiri, Insa akiludira nNyumba Takatifu. Wanu piya wákija naye, iye akikala
nawo, akikola kuwafunda. 3 Wanlimu wa shariya pamoja na Mafarizeu waja
nawo mwanamuka ásinganiwe akizinga. Nakufika, wakimwimisa mbere ya wanu,
4 wakindairi Insa: "Mwanlimu, eyu mwanamuka-yu kakoriwa akizinga. 5 Kwa shariya
yetu ofwe, Musa kâtamuru wanu kamba ewa tiwapanje na mawe. Sambi uwe, ukwamba
mwaja?" 6 Wakindairi javi wamyerere ipate wammonerere ukosa mmojawapo. Insa
akinama, akanza kuremba pansi na cala. 7 Ikisa, kwa kuwa wakizidi kundairi-dairi,
iye akilamuka, akiwambira: "Pamuri-pa, munu saanakola dambi tangu, noyo anze
kulokota riwe ampanje." 8 Mara tena akinama, akizidi kuremba pansi pare. 9 Fala ware
pawasikire javire, wakilawa mmoja-mmoja, ino-ino-ino-ino bila ncocoro. Wanzire
kulawa ndi wazee. Insa wakimwasa nopare, na mwanamuka ire emire novire mbere
yake. 10 Iye akilamuka, akindairi: "Nunu, ewo wandepi? Aabakire-pa anta mmoja
wakusaka kukulaumu?" 11 Akinjibu: "Mwenye, aapo-pa munu anta mmoja." Na Insa
akimwambira: "Nomi novyo sukulamula hukumu. Uka vyako, usikore dambi tena."]

*Mamulaka apewe Insa na Mwenyezimungu*

12 Sambi, Insa akikola kusowera mara nyengine tena na wanu, akiwambira: "Omi
ndi nuru ya mulumwengu-mu. Mwenyé kunifulata omi aashubutu kwenenda nkisi,

† **7:42** Ona Mika 5:2. ‡ **7:53** Mandiko a mida azipo ezi aya-zi 7:53 mpaka 8:11.

ila apata nuru yakumpa mainsha." 13 Kwa javyo, Mafarizeu wakimwambira: "Epa
sambi, uwe kwankulavya ushahidi wako uwe mwanyewe, fala ushahidi wako-wo siwo
bora wakutumainiwa!" 14 Insa akiwajibu, akamba: "Ingawa nilavya ushahidi wangu
omi mwanyewe, fala ushahidi wangu wakweli. Kamana mahala kanilawire na mahala
kanuka nukwijiwa. 15 Umwe mulamula namuna ya kibinadamu. Omi sinlamula munu.
16 Anta panilamula, kulamula kwangu ka shariya kamana omi silamula yeka yangu,
nilamula pamoja na Baba anipereke omi. 17 Anta nkati ya shariya yenu* yandikiwa
kuwa, ikiwa mashahidi wawiri wasema kinu kimoja noco, cawamba-co cakweli. 18 Omi
nilavya ushahidi wangu omi mwanyewe. Baba anipereke-yo alavya novyo ushahidi
wangu omi." 19 Kwa javyo, wakindairi: "Wawayo uwe kawa ndepi?"

Insa akijibu: "Umwe amunijiwa omi caniri na amumwijiwa Baba wangu. Munanijiwa, nanga mumwijiwa novyo Baba wangu." 20 Insa kasowera evi piya-vi ári
nNyumba Takatifu akifunda. Iye ákiwa pansana paikikalanga kashoti ya swadaka ya
Mwenyezimungu. Fala aapo anfungire, konta úkiwa saunafika wakati wake.

### *Insa ndi Mwenye alawire mbinguni*

21 Kwa mara nyengine tena, Insa akiwambira: "Omi nukuka vyangu, umwe mukuja
kunisakula, fala mukufwa na dambi zenu†. Umwe amufika kanuka omi." 22 Ndimana
Mayahudi wakambirana: "Iye akwamba kuwa ofwe atifika kooka iye-po. Iye
vyamba-vi asaka kurulaya?" 23 Insa akiwambira, akamba: "Umwe mulawa pansi-pa
fala omi nilawa julu mbinguni. Umwe muwa wanu wa mulumwengu nomu, omi siri
wa mulumwengu-mu. 24 Omi nukukwambirani kuwa mukufwa na dambi zenu, konta
ikiwa amukubali kuwa omi ndi noyo-noyoni‡, mukuja kufwa na dambi zenu." 25 Kwa
javyo, ewo wakindairi: "Uwe kuwa nani?"

Insa akiwajibu: "Omi ndi noyo wanukwambireni tangu mwanzo. 26 Viwapo vinu
vingi vyawenye vyaníri nawo vyakukuhusuni umwe kukwambirani, na kukulamulani.
Fala anipéreke omi ndi mwenyé ukweli. Vyaninsikire iye ndi vyanukwambirani mulumwengu-mu." 27 Ewo awereriwe kuwa Insa akisowera kuhusu Baba. 28 Kwa javyo,
Insa akiwambira: "Umwe pamusaka kumwimisa pansalaba Binadamu wa Binguni,
basi ndi pamusaka kwijiwa omi caniri. Mukwijiwa kuwa omi Binadamu, na sitenda
kinu kwa mamulaka yangu, ila nisowera vyaanifundire Baba tu basi. 29 Anipéreke-yo
kawa pamoja nomi. Iye aanasire yeka, kamana omi daima nitendanga vyakumwajibu
iye." 30 Wanu wengi pawansikire Insa akisowera javyo, wakinkubali.

### *Mwana wa Iburahima na mwana wa Ibilisi*

31 Kwa javyo, Insa akiwambira Mayahudi wankubalire ware: "Umwe, ikiwa mutenda
vyanukwambireni, kweli-kwelini mukuwa wanafunzi wangu. 32 Umwe mukuja kwijiwa ukweli, na ukweli-wo nowo umwe ukunusuruni." 33 Ewo wakinjibu: "Ofwe tiwa
ujukulu wa Iburahima, tangu atinamba kuwa watwana wa munu. Kutisowerera kuwa
tisakula kunusuriwa sababuni?" 34 Insa akiwajibu: "Nukwambirani kweli kuwa piya
wenye kukola dambi wakuwa watwana wa dambi noyo. 35 Ntwana aana pake kwa
milele, fala mwana wa pakaya kanawo pake kwa milele. 36 Ndimana ikiwa Mwana
akukunusuruni, kweli-kwelini munusurika. 37 Omi nukwijiwa kuwa muwa ujukulu
wa Iburahima. Novyo-sivyo, musaka munulaye, konta usemi wangu amutula mmyoyo
mwenu.

38 Omi nisowera vyanimmonire Baba wangu, umwe mutenda vyamunsikire wawa
yenu." 39 Ewo wakinjibu, wakamba: "Ofwe wawa yetu Iburahima."

Insa akiwambira: "Umwe, munawa wana wa Iburahima, nanga mufulata
vyaákitendanga Iburahima. 40 Fala umwe musaka munulaye, omi níri kukwambirani

* 8:17 "Shariya yenu" ndi Taureti. † 8:21 Mana ake: amuswamiiwe kwa kutowa kutubiya. ‡ 8:24 Epa Insa katumira zina ra Mwenyezimungu, "Omi niwa." Ona Kulawa 3:14.

ukweli waninsikire Mwenyezimungu. Iburahima aatendire javyo. 41 Umwe
mwankutenda vitendo vya wawa yenu.”
Ewo wakimwambira: “Ofwe atiri wana wa zinaa, tanawo wawa mmoja tu basi,
Mwenyezimungu!” 42 Insa akiwambira: “Inawa Mwenyezimungu Baba wenu, umwe
nanga munipenda omi, konta omi nilawa ka Mwenyezimungu, niwa epa. Sirijisire
omi mwanyewe, ila iye ndi anipereke. 43 Umwe amwereriwa vyanukwambirani-vi,
sababuni? Ndi kwa kuwa avikwajibuni kufulata usemi wangu. 44 Umwe wawa yenu
ndi Ibilisi, na umwe vikwajibuni kutenda vimwajibu wawa yenu. Iye tangu mwanzo ki-
somi, enendera njira ya ukweli, konta ukweli wawenye aana. Ibilisi paalongopa, atenda
vitendo vya tabiya yake, kamana iye nlongo, ndi wawa wa walongo. 45 Fala omi, kwa
kuwa nukwambirani kweli, umwe amunikubali. 46 Pamuri-po, nani akidiri kwakikisha
kuwa nanawo dambi? Ikiwa nankukwambirani ukweli, umwe amunikubali sababuni?
47 Ári ka Mwenyezimungu onse, asikiriza caasema Mwenyezimungu. Sababu umwe
amusikiriza ndi kwa kuwa ámuri ka Mwenyezimungu.”

### *Insa ndi mwenyé kuwepo tangu mwanzo*

48 Mayahudi wakinjibu, wakamba: “Atina haki yakukwambira kuwa uwe kuwa
nSamariya, na kwanawo shetwani?” 49 Insa akijibu: “Omi sina shetwani ila ninsifu
Baba wangu, umwe amunisifu. 50 Wala omi sisakula kuritukuza omi mwanyewe.
Kawapo mwengine asakula kutukuziwa kwangu omi, iye ndi mwenyé kulámula.
51 Omi nukwambirani kweli: munu akifulata usemi wangu, kwa milele aayeza kifo.”
52 Mayahudi wakimwambira javi: “Sambi tikwijiwa kuwa uwe kwanawo shetwani!
Iburahima kafwa na minabii wafwa, fala uwe ukwamba, ‘Munu akifulata usemi
wangu, kwa milele aayeza kifo.’ 53 Uwe auri bora wakunzaidi baba wetu Iburahima
afwire? Minabii novyo wafwa. Sambi uwe uritula kuwa nani?” 54 Insa akijibu: “Ikiwa
omi niritukuza mwanyewe, utukufu wangu aufãi kinu. Anitúkuza omi ndi Baba, noyo
wamwámba kuwa ndi Mwenyezimungu wenu-yo. 55 Fala umwe iye amumwijiwa, ila
omi nimwijiwa. Omi nikamba simwijiwa, nukuwa nlongo kamba umwe. Falakini omi
kweli-kwelini nimwijiwa, na usemi wake nifulata. 56 Baba wenu Iburahima kafurahi
konta kejiwa kuwa nukuja. Iye kawona na kawa radi.” 57 Kwa kusema javyo, Mayahudi
ware wakimwambira javi: “Uwe aunatimu myaka amusini. Iburahima-yo kûmmona?”
58 Insa akiwajibu: “Omi nukwambirani kweli: kábula yakupongoriwa Iburahima, omi
niwapo.” 59 Basi wakilokota mawe kusaka kumpanja, fala Insa akirifisa, akilawa
nNyumba Takatifu mure.

# 9

### *Alama yasita yolote vyaári Insa: amponesa munu sawona*

1 Insa paakipita, kammona munu sawona tangu kupongoriwa kwake. 2 Wanafunzi
wake wakindairi: “Mwanlimu, mwananlume-yu kapongoriwa sawona kwa sababu
ya dambi zake au za wawaze?” 3 Insa akiwajibu: “Eyu kutowa kuwona kuno siyo
kwa sababu ya dambi zake wala za wawaze, ila ipate julu yake viwoneke vyaatenda
Mwenyezimungu. 4 Ofwe tijuzi tikore kazi za ire anitumire nsana nowu. Ukuja
usiku saukidirika kukoriwa kazi. 5 Paniri-po mulumwengu-pa, omi ndi nuru ya
mulumwengu-mu.” 6 Nakwisa kusema javire, akisunira pansi, akivulula nsanga ure na
mata, akimpaka* mwananlume ire mmaso, 7 akimwambira javi: “Uka, ukataye kumaso
tanki ulu ya Siloamu.” (Zina ra Siloamu mana ake “kaperekiwa”.) Basi, mwananlume
ire akuka, akitaya kumaso, akiludira ukaya wakuwona wawenye ngwee.
8 Kwa javyo, majirani wake wákimmonanga vyaákiwa, pamoja na wanu wákimmonanga
akipita akilebela zimola, wakamba: “Eyu sinoyu-yu mwananlume ákikalanga akilebela

* **9:6** Kigeregu: “akintawaza”.

zimola-yu?” 9 Wanu wengine wakamba: “Aye, ndi noyu.” Fala wengine wakamba:
“Siye! Eyu kalandana naye tu basi.” Iye akizidi kwamba: “Ndi nomi.” 10 Kwa javyo,
ewo wakindairi: “Sambi, maso ako-yo afunguka mwaja? Uwonaja?” 11 Iye akijibu:
“Mwananlume wakwitiwa Insa ndi avulure nsanga na mata akinipaka mmaso-mu,
akinambira javi: ‘Uka ukataye kumaso Siloamu.’ Nomi nukuka, nikowa, nikanza
kuwona!” 12 Ewo wakindairi: “Noyo mwananlume-yo kawa ndepi?”

Iye akijibu: “Sijiwa.”

13 Ikisa ewo wakintwala mwananlume saâkiwona ire, wakuka naye ka Mafarizeu.
14 Kusema kweli, suku Insa yaâvulure nsanga na mata, akimponesa mwananlume
saakiwona ire, íkiwa suku ya sabadu. 15 Kwa javyo, Mafarizeu ware newo novyo
wakindairi tena namuna vyaaponesiwe awone. Iye akiwambira: “Iye kavulula nsanga
na mata, akinipaka mmaso-mu, ikisa nikitaya kumaso, nikanza kuwona ngwee.”
16 Mafarizeu wamojawapo wakamba: “Eyu munu-yu aaperekiwe na Mwenyezimungu,
kamana aafulata shariya ya sabadu.” Fala wengine wadairi: “Munu mmadambi
atendaja maajuza kamba-ya?” Noparepare wakawanyana. 17 Ndimana Mafarizeu
ware wakindairi saakiwona ire mara nyengine tena: “Kwa kuwa kakufungula maso
ako, kuhusu iye waambani?”

Iye akijibu: “Iye nabii.”

18 Wakulungwa wa Mayahudi ware awakinkubali kuwa aakiwona tangu kupon-
goriwa kwake, akiludira kuwona, mpaka wakiwetisa wawaze mwananlume apone-
siwe ire. 19 Nakufika wawaze, ewo wakiwadairi: “Eyu mwanenu wamwamba kapon-
goriwa sawona-yu? Epa sambi kanza kuwona mwaja?” 20 Wawaze ware wakijibu,
wakamba: “Tikwijiwa kuwa eyu mwanetu, na kâpongoriwa sawona. 21 Fala vyenende
akanza kuwona atijiwa, wala atimwijiwa munu mmojawapo amponese. Iye munu
nzima wawenye, ndairini mwanyewe, akisaka akujibuni!” 22 (Wawaze ware wasowera
javire kwa sababu yakuwopa wakulungwa wa Mayahudi, kamana wakulungwa ware
wâsikizana kuwa wantuwise ndaraja ya nsinagoga munu mmojawapo asáka kuwambira
wenziwe kuwa Insa Almasihi.) 23 Ndimana wawaze ware wajibu javi: “Iye munu
nzima, ndairini mwanyewe!”

24 Kwa javyo, mara yapiri ewo wakimwita mwananlume saakiwona ire,
wakimwambira: “Kwa kutukuziwa Mwenyezimungu, sema kweli yako! Ofwe
tikwijiwa kuwa eyo munu-yo mmadambi.” 25 Akijibu: “Kamba iye mmadambi omi
sijiwa. Canijiwe omi kinu kimoja: ingawa síkiwona, fala sambi nankuwona!” 26 Ewo
wakindairi: “Iye kakutenda kinani? Kakuponesa mwaja?” 27 Iye akiwajibu: “Omi
nûkwambirani futi, fala umwe amusikire. Musaka kusikira tena sababuni? Nomwe
novyo musaka muwe wanafunzi wake?” 28 Ewo wakintukana cwaa, wakamba:
“Epa, uwe kuwa mwanafunzi wake, fala ofwe tiwa wanafunzi wa Musa! 29 Ofwe
catijiwe ndi kuwa Mwenyezimungu kasowera julu ya Musa, fala kuhusu eyu,
atimwijiwa anta upande waalawirire!” 30 Mwananlume ire akiwajibu, akamba:
“Mama! Mbana vishangisa! Umwe amwijiwa kalawirira, fala iye omi kaniponesa.
31 Tikwijiwa kuwa Mwenyezimungu aawasikiriza wamádambi, fala awasikiriza wenye
kumwishimu, watimiza vyaasaka iye. 32 Tangu mwanzo wa ulumwengu, hapana
manziro kasikirikana kuwa munu mmojawapo kamponesa munu waâkupongoriwa
sawona. 33 Inawa eyu munu-yu aajire kulawa ka Mwenyezimungu, aangari kutenda
kinu kamba-ci.” 34 Ewo wakinjibu: “Uwe kuwa mmadambi nfululu! Sambi, uyerera
kutifunda ofwe mwaja?” Noparepare wakintuwisa wakinlavira panja ya sinagoga ire.

35 Insa paasikire kuwa wantuwisira panja, akinsingana mwananlume ire, akindairi:
“Uwe, unkubali Binadamu wa Binguni?” 36 Mwananlume ire akijibu, akamba: “Noyo
nani, Mwenye? Nambire, ipate ninkubali!” 37 Insa akimwambira: “Uwe kummona,

ndi noyu-noyuni wauri kusowera naye sambi-pa-yu!" 38 †[Iye akamba: "Mwenye,
nukwamini!" Naye akimwabudu. 39 Insa akimwambira:] "Omi nija mulumwengu-mu
niwalamure wanu. Nija ipate vipofu wawone, na wawona wawe vipofu." 40 Mafarizeu
wengine waákiwa nawo karibu iye wansikire akisowera javire, wakindairi: "Epa,
ikuwa ofwe novyo tiwa vipofu, nikamba?" 41 Insa akiwajibu: "Inawa umwe muwa
vipofu, amungari kuwa na wamádambi! Fala kwa kuwa mukwamba 'Tiwona', salani
na madambi yenu."

# 10

*Insa ndi Nryango na Nsunga mwema*

1 Insa kazidi kusowera, akamba: "Omi nukwambirani kweli. Akwéra sereka ya
makondoo onse, kwasa kupita panryango, noyo-noyoni mwivi na nnyang'anyi. 2 Fala
apíta panryango onse, ndi nsunga wa makondoo. 3 Kwake iye nakola wa panryango
wa sereka ndi afungúla nryango. Makondoo wamanyira shauti yake. Aweta makondoo
mazina awo, newo awasungira panja. 4 Bandi yakuwalavira piya panja, iye alongorera.
Makondoo wanfulata konta wamanyira shauti yake. 5 Munu sawamwijiwa awanfulata
ila wantira, konta awamanyira shauti za wanu sawawejiwa." 6 Insa wanu ware
kawasowerera eci kinyume-ci, fala ewo awereriwe mana ake vyawambiriwe vire.

7 Kwa javyo, Insa akiwambira tena: "Nukwambirani kweli. Omi ndi nryango ka
makondoo. 8 Piya walongorere kábula ya omi wevi na wanyang'anyi, na makondoo
awawasikirize. 9 Omi ndi nryango. Anipíta akingira julu yangu omi onse, avushiwa.
Kanawo mahala pakutumaini.* 10 Mwivi aaja sairi kuja kwiwa, kuulaya na kudangula.
Omi nija ipate wawe na mainsha, wawe nawo pakulu pawenye."

11 Insa akizidi kusowera, akamba: "Omi niwa Nsunga mwema. Nsunga mwema
apereka mainsha ake afwe kwa ajili ya makondoo wake. 12 Nsunga wakupokeresiwa,
nsunga-yo makondoo siwakewakeni. Iye siyo nsunga wa kweli. Ndimana, akimmona
mmwinzi akija, atuwa, awasa makondoo. Basi mmwinzi anduru kondoo mmoja,
wengine watawanyikana. 13 Kwa kuwa nsunga wakupokeresiwa aawashugulikira
makondoo. 14 Omi niwa Nsunga mwema. Niwejiwa makondoo wangu, newo omi
wanijiwa, 15 kamba Baba vyanijiwa, nomi nimwijiwa Baba. Omi nipereka mainsha
angu nifwe kwa ajili ya makondoo wangu. 16 Nanawo makondoo wengine sawapo eci
kitundu-ci, newo novyo nijuzi niwalongoze. Ewo wakuja kusikira shauti yangu. Kwa
javyo, uwapo nfuwo moja na nsunga mmoja. 17 Baba anipenda kwa kuwa nipereka
mainsha angu nifwe, niludire kutwala tena. 18 Hapana alávya mainsha angu, ila omi
niripereka mwanyewe nifwe. Nanawo mamulaka a kupereka, na nanawo mamulaka
a kupewa kupokerera tena. Ndi vyanilaiziwe na Baba wangu."

19 Kwa mara nyengine tena, kukilawirira kwawanyana nkati ya Mayahudi kwa
sababu ya nowu usemi-wu. 20 Wengi wakamba: "Iye kapatiwa na shetwani,
kangamiya! Noyu munsikiriza sababuni?" 21 Wengine wakamba: "Usemi-wu siwo wa
munu wakumilikiwa na shetwani. Shetwani amponesa munu sawona?"

*Insa na Baba kinu kimoja*

22 Nowo wakati-wo, Yerusalemu ritendiwa Jambo ra Nyumba Takatifu†. Úkiwa wakati
wa baridi. 23 Insa akipita akenenda nlupenu ra Nyumba Takatifu, lupenu-ro rikitiwa
"Lupenu ra Selemani". 24 Mayahudi wakijumana wakinzunguriza wakindairi: "Uwe
kwankutangaisha mpaka rini? Tambire kweli kamba uwe kuwa Almasihi, au auri?"
25 Insa akiwajibu: "Omi nûkwambirani futi fala amusaka kukubali. Kazi zanitenda

† **9:38** Atina uhakika aya 38 na 39 kuwa ziwapo mmandiko matanzi. * **10:9** Kigeregu: "Akwingira, alawa, na apata cakurya." † **10:22** Jambo-ri anzima yake íkiwa kukumbukira suku yakunshukuru ka Mwenyezimungu kuhusu Nyumba Takatifu nyipya.

omi kwa zina ra Baba zikolota ushahidi caniri omi. 26 Fala umwe amukubali konta
ámuri makondoo wangu. 27 Makondoo wangu wasikira shauti yangu. Omi niwejiwa,
newo wanifulata. 28 Omi niwapa mainsha a milele, awapoteya tena. Hapana akidíri
kunipokonyola mmakono mwangu. 29 Baba wangu anipére ewo ndi bora pakulu
kupunda piya. Hapana akidíri kumpokonyola Baba mmakono mwake.” 30 Omi na Baba
tiwa kinu kimoja.

31 Mayahudi mara nyengine tena wakilokota mawe wampanje. 32 Insa akiwambira:
“Omi nukoloterani kazi nyingi ngema za Baba. Kazi mojawapo yamusaka kunipanjira
ndi yepi?” 33 Mayahudi wakinjibu: “Atisaka kukupanja kwa sababu ya meema
yautendire, ila kwa namuna zako zakukufuru! Konta uwe kuwa mwanadamu, fala
uritula kuwa Mwenyezimungu!” 34 Insa akiwajibu: “Yandikiwa nkati ya shariya
yenu‡ kuwa Mwenyezimungu kâmba javi: ‘Umwe muwa milungu.’ Sikweli? 35 Iye
kaweta ‘milungu’ ware wapokerere habari za Mwenyezimungu, (na Mandiko aapin-
duka). 36 Kwa javyo, ire atawáziwe na Baba, akiperekiwa mulumwengu-mu, mwamba
kuwa iye kankukufuru kwa sababu nukwamba: ‘Niwa Mwana wa Mwenyezimungu’.
Mwaja? 37 Ikiwa sitenda kazi za Baba, musinikubali. 38 Fala ikiwa nankutenda kazi
za Baba, anta musinikubali omi-pa, kubalini kwa kazi zanitenda, ipate mwijiwe na
mwereriwe sana-sana kuwa nilungana na Baba na Baba kalungana nami.”

39 Kwa mara nyengine tena wayerera kunfunga, fala iye akiwapolonyoka mmakono
mwawo. 40 Iye akuka vyake tena, akiloka muto wa Yordani, akuka mpaka mahala
paânzire Yahaya koza, akikala nopare. 41 Wanu wengi wawenye wakija kwake iye,
wakamba: “Yahaya aatendire alama anta mamoja, fala piya vyaambire kuhusu eyu
mwananlume-yu vyakweli!” 42 Basi nokurekure, wanu wengi wawenye wankubali
Insa.

# 11

*Alama yasaba yolota vyaári Insa: anfufula Lazaru ka wafwi*

1 Ákiwapo mwananlume mmoja wakwitiwa Lazaru ákiwa nlwere. Iye kwawo kúkiwa
Betaniya, kaya yawákikalanga Mariyamu na Marta nduye. 2 Mariyamu noire âmmiminire
sheru Mwenye, ânfutire mmaulu na nywiri zake ire, nlumbuwe wakwitiwa Lazaru
ndi ákiwa nlwere. 3 Basi walumbuze ware watumiza kumwambira Insa: “Mwenye,
waumpenda uwe-yo kuno umpata ulwere.” 4 Fala Insa paasikire javire, akamba: “Ewo
ulwere-wo mwinsho wake siyo kufwa ila wolote utukufu wa Mwenyezimungu. Julu ya
ulwere-wo atukuziwe Mwana wa Mwenyezimungu.”

5 Sambi, Insa akiwapenda pakulu sana Marta na nduye pamoja na nlumbwawo
Lazaru. 6 Kwa javyo, paasikire habari yakuwa Lazaru nlwere, Insa akikala tena suku
mbiri kaákiwa nokure. 7 Ikisa akiwambira wanafunzi wake: “Tukeni tiludire tena
Yudeya.” 8 Wanafunzi ware wakimwambira: “We! Mwanlimu! Mayahudi suku mbiri-
nozizi noko wákisaka kukupanja na mawe, sambi uludira kuka tena noko mwaja?”
